# Mwongozo wa mwalimu

## Wakati wa biblia Kiwango 1 na 2

Msururu A
Masomo 1 - 6

www.besweb.com

## Bible Educational Services

Registered Charity UK (No 1186004)

**Misheni yetu**

Kutunga mafundisho ya Biblia kwa walimu ili  wafundishe ukweli wa Yesu Kristo kwa kizazi kinachokuja katika dunia yote.

**Vision Statement**

Kufikia kizazi kinachokuja na ufahamu wetu wote katika lugha zao kwa kuendeleza na kusaidia shirika la kimataifa la washiriki waliojitolea.

## HABARI KWA JUMLA

**Kazi inayofanywa na Bible Educational Service:**

Kazi ya mafundisho ya kibiblia (Bible Educational service) inachapisha katika kingereza mafundisho ya Biblia “Bibletime”’, “New Life” na “Gleaner”. Inasaidia vituo vya usambazaji wa mafundisho hii na kila shirika ya namna hiyo inayozitumia katika Uingerezana na pahali pengine duniani, kwa njia ya kuwatembelea, kuwashauri, na wakati wa kuwafundisha. Katika inchi mbalimbali, Bes iliendeleza pia ushirikiano na vikundi nyingi vinavyofanya kazi ya utafsiri, muundo, uchapishaji na usambazaji wa mafundisho. Kila mara inapewa bure kwa wote.

Mafundisho “wakati wa biblia” ilianza pale Irland tangu miaka zaidi ya 50. BES iko na hati miliki ya mafundisho katika kiingereza vilevile katika lugha zote zingine. Sehemu kubwa ya mafundisho hii imechapishwa katika muundo wa A4 na inatumiwa kama mafundisho kwa mfano wa barua katika inchi nyingi zinazozungumza Kiingereza. Kama inajazwa na watoto, masomo inarudishwa, baada ya kila wiki ine, katika kituo kimoja ili ipewe pointi (Bible school Center). Tangu muda mfupi, mafundisho imechapishwa pia katika vitabu vya muundo wa A5, vilivyo na mafundisho ya miezi sita, kupitia Revival Movement katika Irland ya kaskazini. Hii iliwezesha kabisa utumizi wake katika ma kanisa na shule, zaidi katika eneo ambako kazi ya posta haipo tena.

Mafundisho ya BES inapatana pia vema na utumizi wa kibinafsi nyumbani ao katika kundi, ikiwa ndani ya ma kanisa ao ndani ya ma shule. Programu iliyotungwa inawezesha watoto na vijana kuendelea kujifunza Biblia muda wa zaidi ya miaka kumi. Viwango tano vya masomo vinapatikana sasa katika kingereza (miaka 3 - 4, miaka 5 – 7, miaka 8 - 10, miaka 11 – 13, miaka 14 – 16). Kwa kila mmoja wao, programu inachukua miaka tatu. Mtoto ao kijana anaweza kujifunza viwango tofauti kulingana na uwezaji wake kibinafsi. “Wakati wa biblia” inaleta kwa watoto na vijana nafasi kwa kujifunza Neno la Mungu, kujifunza hadisi za Biblia na kuelewa maana ya injili katika maisha yao wenyewe.

Mafundisho inayopatikana katika ufaransa inaweza kuchapishwa kutoka tovu – www.besweb.com – ao kwa kumuomba katibu wa kimataifa. Inapatikana pia kwa lugha zingine katika tovu. Pia kuna vitabu vingine ambavyo vinaweza kuwa vya muhimu kwa inchi mpya ao maeneo inayotaka kuanzisha kituo cha BES.

## Anuani ya kufaa:


**UK (Northern Ireland) Office(ghala za masomo zote)**
37a Belmore Street, Enniskillen, Northern Ireland BT74 6AA
Phone: 0286 632 2462

**UK Katibu**
Mr Stephen Gillham,
Email: stephen.gilllham@besweb.com

Site web: www.besweb.com
Email: info@besweb.com

## MWONGOZO WA MWALIMU

Katika mwanzo, mafundisho ya “Wakati wa Biblia” ilitolewa kwa mfano wa mafundisho kwa njia za barua kwa ushirikiano na kituo kimoja cha “shule ya Biblia kwa njia ya posta”. Lakini, zaidi na zaidi mafundisho hii inasomwa pahali ambapo kazi ya posta siyo ya kuaminika, hasa katika shule na ma kanisa katika Afrika, India na pahali pengine. Mwongozo wa mwalimu uko pale kwa kusaidia wale wanaotumia mafundisho katika mazingiza kama haya. Kitabu hiki kinatungwa juu ya kuwa mwongozo wa kiwango 1 na 2, ambavyo vinakusudiwa watoto kutoka umri wa miaka 5 hadi 10.

Maelezo ya mwongozo huu yanafuata maandiko ya Biblia ambayo ni namna moja na ile iliyo katika mafundisho yenyewe. Mafundisho, na maelezo, imetungwa mu namna ya somo moja kwa wiki. Kwa hiyo, masomo katika Aprili inaambatana na Pasaka na masomo katika Desemba inaambatana na Krismasi.

Kulingana na pahali, ao masomo kwa wiki katika muundo wa A4, ao vitabu vya muundo wa A5 ambamo muna masomo 24 kwa miezi 6, vitatumiwa. Ni mwalimu ndiye atagawa masomo A4 kwa mwezi. Kila wiki kartasi itajazwa kwenye kanisa ao shule, ao itapelekwa kwa mtoto na kurudishwa yenye kujazwa, baada ya wiki moja. Mwisho wa kila mwezi, mwalimu atachukua masomo na ataipatia ma pointi; atairudisha kwa wanafunzi yenye kurekebisha, na haraka iwezekanayo.

Iliyo vema, vitabu vya muundo wa A5 vinapaswa kuchukuliwa na kupewa ma pointi mwisho wa kila mkutano, lakini mara nyingi tunaona kwamba haiwezekane. Katika kesi hii, ni vema kuigawa kwa wanafunzi wengine, na mwalimu ataleta ma pointi kwa masomo akisema kwa sauti na wakati wanafunzi watakuwa wanarekebisha na kuweka alama katika masomo ya wenzao. Katika ukurasa wa mwisho wa kila kitabu, kuna fasi ambayo inaruhusu kuandika kiwango cha kufaulu cha kila mwezi, na pia maoni kuhusu maendeleo ya mwanafunzi. Kwenye cheti hiki inaonekana nambari ya kiwango cha kufaulu kwa mwanafunzi muda wa miezi sita ya masomo.

## MASHAURI YA MUHIMU KWA WALIMU

Hapa, lengo siyo kwamba ni maagizo kwa walimu na kuwanyima uwezekano wote wa kulinganisha somo, kufuatana na mawazo na mipango yao wenyewe. Ni mapendekezo tu ambayo inaweza kusaidia katika utumizi wa mafundisho ya “wakati wa Biblia”.

- **Kujua historia vizuri –** Mwalimu anapaswa kufanya yote iwezekanayo ili ajue vizuri historia ya Biblia, vilevile mafundisho ya “wakati wa Biblia” ambayo inaambatana nayo. Iliyo vema ni kwamba amalize yeye mwenyewe kujifunza somo kabla ya kuwaambia watoto. Maelezo ya mwongozo inapaswa pia kusomwa na uangalifu kwa kusaidia katika kupangwa kwa kila somo.
- **Kuelewa mafundisho ya kushika –** Juu ya kila ukurasa, unaweza kusoma: “tunajifunza kwamba”, inafuatiwa na nukta mbili kubwa ambayo tunatumaini kwamba watoto wataelewa kisha kusikia maelezo ya mwalimu na kisha kujifunza mafundisho ya “wakati wa biblia”. Nukta kubwa ya kwanza inaelekea ufahamu na uelewa wa historia. Ya pili inatia watoto moyo kwa kushika kibinafsi mafundisho inayopatikana katika historia hiyo. Ma nukta kubwa hii ya kushika inafanya muhtasari wa ukweli muhimu ambao ulifundishwa katika somo. Mwalimu anaweza kuitumia kwa “kujipima kibinafsi” kutokana na mafundisho iliyopewa, pia uelewa wa watoto.
- **Kutanguliza –** Mafundisho yote inaanza kwa kuambatanishwa na mambo ambayo watoto wenyewe waliishi, inayofanana na jambo ambayo inaelezwa katika historia. Mawazo mengi yamependekezwa juu ya kutanguliza hadisi na kuwezesha watoto wajifunze kwa bidii tangu mwanzo wa huu wakati wa mafundisho ya Biblia.
- **Kufundisha –** Ma nukta kubwa za historia zimetajwa. Tunatumaini kwamba mwalimu hatakuwa anaisoma wakati anaieleza. Lakini, lazima ajue vizuri historia ili aweze kuisema kwa bidii na kuamsha akili. Atafanya kwamba wanafunzi waelewe mafundisho kubwa ya kushika na atawaongoza katika jinsi wanaweza kujibu na kuitumia. Tulijaribu, ilivyowezekana mara kwa mara kutoa maelezo fulani wakati historia inapoelezwa. Hiyo inaonekana kila mara katika maandishi ya *italiki*.
- **Kujifunza –** Kila historia inaambatana na shairi muhimu. Wakati mwingine kuna mbili, kama ya pili iliongezwa, inaweza kuwa mwepesi kukamata katika akili. Tunatumaini kwamba watoto watajifunza vizuri ma shairi muhimu na mara kwa mara watakuwa na nafasi kwa kuirudia juu ya kuikumbuka vema.
- **Kujaza somo –** Ikiwa masomo inafundishwa katika shule, mwalimu atajua kama watoto wanaweza kujaza masomo pekee ao kama wanahitaji kusaidiwa. Ikiwa ni lazima, inapaswa mwalimu awasomee maandiko ya somo watoto wengine ambao hawataweza kusoma pekee. Katika kesi moja kama katika nyingine, inaweza kuwa ya mafaa <u>kuamsha akili</u> ya wanafunzi katika ma nukta moja ambayo inapatana na maswali. Kama

mafundisho ya “wakati wa biblia” inatumiwa katika mazingira ingine isiyokuwa shule, ni ya muhimu kwamba mwalimu awe mwema na tayari kusaidia watoto ili mafundisho hii isionekane kuwa kitu cha magumu na cha kuchokesha, lakini kwa tofauti ionekane kuwa wakati wa kufurahisha. Ni ya muhimu pia kuwatia moyo watoto na kuwapongeza wakati wanapojifunza.

- **Kurudia –** Maswali na / ao michezo kidogo imepewa juu ya kurahisisha majifunzo na marudio ya historia.
- **Kuonyesha –** Katika ma kesi nyingine, tunajua kwamba inaweza kuwa magumu kuwa na vyombo vya kuonyesha picha. Lakini ikiwezekana, ni ya muhimu sana kuonyesha picha ao vitu ambavyo vitasaidia watoto kuelewa historia kwa njia ya mifano. Tunakushauri kutembelea tovu www.freebibleimage.org ambayo inaleta picha nyingi ya ajabu ya historia ya biblia. Kuandika tu jina ya yule aliye katika historia, katika kiingereza (kila mara), kwa mfano “Noah and the Ark”, msururu mzima wa ma picha inayomuelekea inaweza kupakuliwa kwa bure. Eikon Bible Art (www.eikonbibleart.com) inaleta pia vyombo vya kuonyesha picha lakini vifaai vyake ni vya kuuza. Ikiwezekana, mifano iliyo katika mafundisho ya “wakati wa biblia” inaweza kunenepeshwa na fotokopi, kisha kuwekwa rangi na kutumiwa kwa kuonyesha picha.

## Kufundisha mstari muhimu

Shairi inaweza kuandikwa katika karatasi kubwa ao katika kibao. Kisha, maneno mengi inaweza kuondoshwa polepole wakati watoto wanatamka shairi, mpaka wakati hakutabaki tena neno hata moja na wafikie kutamka shairi yote mzima, bila kusaidiwa.

Kwa kutanguliza mstari muhimu unaweza kutumia:

1. Mchezo wa kujaza visanduku: Mstari muhimu inaandikwa na herufi nyingi ambazo zinakosekana, hakuna neno inayo herufi zote. Watoto wanapendekeza herufi juu ya kujaza ma tundu, mpaka wakati mmoja wao anatambua shairi.
2. Kila mtoto eko na Biblia na wote wanafukuzia ili wavumbue shairi wa kwanza. Wa kwanza kuipata lazima aisome kwa sauti kubwa.

## Kusimamia muda

- Maelezo yote yameundwa namna moja, ikilinda taratibu moja ya sehemu tofauti. Lakini ikiwa ya lazima, mwalimu anaweza kubadilisha muundo.
    1. Kueleza na kufundisha historia: Karibu dakika 15,
    2. Kujifunza

    Mstari muhimu: karibu dakika 5 mpaka 10

    3. Kujaza karatasi: dakika 20
    4. Michezo na ma kazi nyingine: dakika 5 mpaka 10.

Kumbuka haya:

“Uniambie na mimi nitasahau,
Unionyeshe na nitakumbuka,
Unishirikishe na nitaelewa”

## Kitabu cha Wakati wa Biblia

| | Hatua ya 1 (miaka 5-7)<br>Hatua ya 2 (miaka 8-10) | Hatua 3 (miaka 11-13) | Hatua 4 (miaka 14+) |
|---|---|---|---|
| MSURURU A | 1. Uumbaji<br>2. Noa<br>3. Petro<br>4. Petro/Msalaba<br>5. Abrahamu<br>6. Abrahamu<br>7. Petro<br>8. Petro<br>9. Yakobo<br>10. Wakristo wa kwanza<br>11. Paulo<br>12. Historia ya Krismas | 1. Uumbaji<br>2. Noa<br>3. Petro<br>4. Petro/Msalaba<br>5. Petro<br>6. Abrahamu<br>7. Yakobo<br>8. Maombi<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Historia ya Krismas | 1. Uumbaji na kuanguka<br>2. Mwanzo<br>3. Petro<br>4. Petro/Msalaba<br>5. Petro<br>6. Abrahamu<br>7. Yakobo<br>8. Maisha ya kikristo<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Historia ya Krismas |
| MSURURU B | 1. Utoto wa Kristo<br>2. Miujiza<br>3. Betania<br>4. Msalaba<br>5. Mafumbo<br>6. Yosefu<br>7. Yosefu<br>8. Yesu anakutana na watu<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Historia ya Krismas | 1. Mafumbo<br>2. Miujiza<br>3. Betania<br>4. Msalaba<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yosefu<br>7. Yosefu<br>8. Waandishi wa Injili<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Historia ya Krismas | 1. Mafumbo<br>2. Miujiza<br>3. Betania<br>4. Bwana Yesu<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yakobo na familia yake<br>7. Maisha ya Yosefu<br>8. Njia ya kwenda<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Sheria<br>12. Muujiza wa Krismas |
| MSURURU C | 1. Danieli<br>2. Miujiza ingine<br>3. Miujiza ingine<br>4. Historia ya pasaka<br>5. Ruta na Esiteri<br>6. Daudi<br>7. Daudi<br>8. Yosua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Yona<br>12. Historia ya Krismas | 1. Danieli<br>2. Miujiza ingine<br>3. Miujiza ingine<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruta<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8. Yosua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu waliotumiwa na Mungu<br>12. Historia ya Krismas | 1. Danieli<br>2. Maneno ya Yesu ine<br>3. Nguvu ya Bwana<br>4. Bwana Yesu<br>5. Ruta<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8. Yosua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu wa Agano la Kale<br>12. Kuzaliwa kwa Kristo |

## A1 SOMO 1
**Mungu anaumba dunia**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Mungu aliumba dunia<br>• Tunapaswa kumshukuru Mungu kwa yote aliyofanya<br><br>**Mstari muhimu:** ***Mwanzo 1:1***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 1:1-19*** |
| **KUTANGULIZA** | • Onyesha picha ya nyumba ao uwaombe watoto wachore nyumba<br>• Uliza watoto maswali kuhusu nyumba. Itachukua muda gani kwa kuijenga? Ni vifaa gani vitahitajika?<br>• Inahitaji vifaa nyingi kwa kujenga nyumba, lakini Mungu aliweza kuumba ulimwengu bila kitu. |
| **KUFUNDISHA** | • Katika Mwanzo Mungu aliumba mbingu na dunia. Mbele ya hivyo, kulikuwa tu giza. ***(Mwanzo 1:1-2)*** *Ingekuwaje, kama kungekuwa giza kila wakati? (Unaweza kufunika macho ya mtoto moja na sanda, juu ya kuonyesha mfano wa hiyo).*<br>• Siku ya kwanza, Mungu akasema: “Nuru iwe!” Na nuru ilikuwa. Mungu akaita nuru Mchana na giza aliita usiku. Tangu sasa, si giza la kudumu tena, lakini ubadilishaji wa giza na nuru. ***(Mwanzo 1:3-5)***<br>• Siku ya pili, Mungu akasema tena na aliumba mbingu na hewa inayozunguka dunia. Ilikuwa mangaribi na ilikuwa mwisho wa siku ya pili. ***(Mwanzo 1:6-8)*** *Uwaambie watoto wapumue kwa nguvu sana. Eleza jinsi hewa iliyo kando kando yetu ni ya muhimu.*<br>• Mpaka hapo, dunia ilikuwa imefunikwa na maji, lakini wakati ulitimia sasa wa kuumba inchi kavu, iliyo kavu. Mungu akasema kwamba maji yakusanyike na iache inchi kavu ionekane. Maji yamekuwa ma bahari ambayo inafanya mipaka ya ma bara. Kisha Mungu akasema tena : “Inchi itoe majani, mboga ikitoa mbegu..., miti ya wa matunda.” Mungu aliona ile yote alifanya na akaona kwamba ilikuwa vema. Ilikuwa siku ya tatu. ***(Mwanzo 1:9-13)*** *Uwaambie watoto wataje ma jina ya miti inayoota katika maeneo yao. Kuzungumza juu ya aina mbalimbali za rangi, umbo na urefu. Kuwakumbusha kwamba miti ni nzuri na ya muhimu.*<br>• Siku ya ine, Mungu alifanya miangaza juu ya kuangazia mbingu: jua juu ya mchana na mwezi na nyota kwa ajili ya usiku. Mungu akaona miangaza ambayo aliumba na aliona kwamba ilikuwa vema. ***(Mwanzo 1:14-19)****. Kuzungumza juu ya faida ya jua. Kushangaa juu ya kiwango kubwa cha wingi wa nyota!*<br>• *Kuwaelezea watoto kwamba Mungu aliumba dunia nzuri pamoja na yote ambayo tunahitaji na kwamba tunapaswa kumushukuru kwa hiyo.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Mwanzo 1:1***. Kueleza maana yake ikiwa ni lazima. |
| **KURUDIA** | • Dunia ilikuwa je katika mwanzo?<br>• Nuru ilionekana siku gani ?<br>• Siku ya pili, Mungu aliumba mbingu na ........ .<br>• Katika mwanzo, nini ilifunika dunia ?<br>• Siku ya tatu, ni vitu gani viwili ambavyo Mungu aliumba na vinachipuka ?<br>• Ni mwangaza gani ambayo Mungu aliumba kwa ajili ya mchana ?<br>• Ni miangaza gani ambayo Mungu aliumba kwa ajili ya usiku ?<br>• Jaza mstari huu : “Katika mwanzo, Mungu aliumba...” |

**A1 SOMO 2**
**Mungu anaumba wanyama na mwanadamu**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Mungu aliumba watu kwa mfano wake na weko na bei kubwa kwake<br>• Tunapaswa kufuata njia za Mungu sababu alituumba.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Mwanzo 1:31***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 1:20-2:3*** |
| **KUTANGULIZA** | • Leta kitu moja ambacho ulifanya lakini ulishindwa, kwa mfano mkate uliochomwa kabisa. Sema kuhusu kukatishwa tamaa kwetu wakati mambo hayaendi vile tulitarajia.<br>• Kuwaambia watoto kwamba Mungu alifanya wanyama wengi tofauti na hakuna hata moja wao ambaye alimkatisha tamaa.<br>• Ao tena watoto wanaweza kuiga wanyama mbalimbali (wengine wanaweza kuvumbua ni nyama gani). |
| **KUFUNDISHA** | • Siku ya tano, Mungu alifanya ma elfu na ma elfu za wa ndege na samaki mbalimbali. Aliona kila kitu alichofanya, na alisema: “ni kizuri sana.” ***(Mwanzo 1:20-23)*** *Zungumzia ndege na samaki fulani wengine wale kundi lako la watoto linajua.*<br>• Siku ya sita, Mungu akafanya nyama zote. Akamfanya Twiga na shingo lake mrefu, pia Simba na Chui na meno yao yenye chongo. Mungu aliwaumba wote. ***(Mwanzo 1:24-25)***<br>• Ingawa Mungu amekwisha kuumba vitu nyingi vya ajabu, kulibaki tena kitu kingine cha kufanya, na hiki, alikifanya mu namna ya pekee. *Kuonyesha watoto fungu la udongo na kuwauliza ni nini wanawaza kuweza kufanya nayo.* Mungu alichukua mavumbi ya udongo na alifanya nayo mtu wa kwanza. Mtu alikuwa kiumbe chenye uhai wakati Mungu alipopuliza pumzi ya uzima katika pua zake. Mtu wa kwanza aliitwa Adamu. ***(Mwanzo 1:26-31)*** *Kuwaambia watoto kwamba wakati Mungu aliumba Adamu, alimfanya kwa mfano wake yeye mwenyewe. (vile yeye eko) kama mfano. Ile inamaanisha kwamba Mungu aliumba mtu ili amuwakilishe kwa njia fulani. Kwa sababu tuliumbwa kwa mfano wa Mungu, sisi ni tofauti na wanyama. Tunaweza kufanya mambo na kufikili. Ile inamaanisha pia kwamba tunajua tofauti iliyo kati ya uzuri na ubaya, na tunaweza kujifunza kufuata Mungu na njia zake.*<br>• Mungu aliumba dunia na vyote vilivyomo kwa siku sita. Wakati alipomaliza alisemea kwamba vilikuwa vizuri sana. Siku ya saba, alipumzika na kupendezwa na uumbaji wake wote. ***(Mwanzo 2:1-3)*** *Zungumzia hitaji letu la sisi kupumzika baada ya kufanya kazi nyingi.*<br>• • *Kwa kumaliza, uwakumbushe kwamba dunia iliyoumbwa na Mungu ilikuwa kamilifu, na aliona kwamba yote ambayo aliumba ilikuwa vizuri sana.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Mwanzo 1:31***. Kueleza maana yake ikiwa ni lazima. |
| **KURUDIA** | • Ni sIku ya ngapi Mungu aliumba ndege na samaki?<br>• Mungu alisema nini juu ya hivyo?<br>• Mungu alifanya nini siku ya mwisho, zaidi ya wanyama?<br>• Mungu alisema nini katika mwisho wa kuumba?<br>• Ni nani alikuwa mtu wa kwanza?<br>• Mungu alichukua nini kwa kumuumba?<br>• Mungu aliumba dunia kwa siku ngapi?<br>• Mungu alifanya nini siku ya saba? |

<u>A1 SOMO 3</u>

**Mwanaume wa kwanza na mwanamke wa kwanza**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Mungu alimuumba mwanamke kwa ajili ya Adamu ili amsaidie kutunza uumbaji.<br>• Mungu anatawala kila kitu.<br><br>**Mstari muhimu:** ***ao Mwanzo 2:18, ao Zaburi 24:1***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 2:4-25*** |
| **KUTANGULIZA** | • Ikiwa watoto wanajua bustani ni nini, zungumzia kuhusu vitu ambavyo wanaweza kuona vinachipuka humo, ao onyesha mimea ya eneo lenu. Ikiwa neno bustani ni kitu kipya kwa watoto, eleza tu kwamba ni pahali ambapo watu wanalima mimea, mboga, maua, na kazalika..., pia jaribu kueleza inaweza kufanana na nini.<br>• Eleza kwamba bustani ya Edeni ilikuwa muzuri sana Zaidi ya chochote tunaweza kuchora ao hata kuwaza.<br>• Zungumzia bustani ya Edeni. Ungependa kuishi humo? Ungependelea nini wewe? Unawaza kwamba Adamu alijisikia kuwa pekee? |
| **KUFUNDISHA** | • Adamu aliishi katika bustani nzuri inayoitwa Edeni. Pale, Mungu alimpa Adamu kila kitu alichohitaji. Chakula na maji. Mungu alimuomba pia Adamu atunze bustani. ***(Mwanzo 2:15)***<br>• Mungu alimuonyesha Adamu wanyama wote alioumba. Adamu aliwapa kila mmoja wao jina. ***(Mwanzo 2:19-20)***<br>• Mungu hakutaki Adamu abaki pekee. Hata hivyo, alizungukwa na wanyama wazuri, na ndege, na miti pia mimea, lakini Mungu alijua kwamba alihitaji mtu wa kipekee ambaye ataishi naye pamoja katika bustani. Mungu alileta usingizi mzito kuangukia Adamu, na wakati alikuwa amelala, aliumba mwanamke wa kwanza kwa ubavu wa Adamu. Hivyo, hakuwe tena pekee. Sasa, alikuwa na mke anayeitwa Eva, mwenziwe wakati alikuwa anatunza bustani ambayo Mungu alimpa. ***(Mwanzo 2:20-24)***<br>• Kulikuwa miti nyingi katika bustani. Katikati ya bustani, kulikuwa mti ulioitwa “mti wa kujua uzuri na ubaya.” Mungu aliwaambia Adamu na Eva kwamba walikuwa na ruhusa ya kula matunda yote ya bustani, ila tu tunda ya “mti wa kujua uzuri na ubaya.” ***(Mwanzo 2:16-17)*** *Zungumzia ma kanuni ambayo watoto wanajua kwao ao shuleni. Kwa nini tunahitaji ma kanuni? (kwa ajili ya kuwa katika salama na furaha.) Angalia kama watoto wanaelewa vizuri kanuni ambayo Mungu anawaomba Adamu na Eva waheshimu.*<br>• *Eleza kwamba Mungu aliumba dunia na anatawala juu yake, kumbe inaonekana kwamba yeye tu anaweza kuamua namna wanadamu wanapaswa kuishi humo. Sisi pia, tunapaswa kuheshimu ma kanuni.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Mwanzo 2:18, ao Zaburi 24:1*** Kueleza maana yake ikiwa ni lazima. |
| **KURUDIA** | • Adamu aliishi wapi?<br>• Adamu alipaswa kufanya nini katika bustani?<br>• Ma jina ya wanyama inatoka wapi?<br>• Jaza sentensi hii: Mungu alitaka kuumba ........... kwa ajili ya Adamu<br>• Mungu alichukua nini ili amuumbe mke wa Adamu?<br>• Mke wa Adamu aliitwa je?<br>• Mti wa kipekee katika bustani uliitwa kwa jina gani?<br>• Ni kanuni gani ambayo Mungu alileta kuhusu »mt iwa kujua uzuri na ubaya”? |

## A1 SOMO 4
**Dunia ya Mungu imeharibika**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Adamu na Eva hawakumtii Mungu na kwa hiyo waliharibu uumbaji wake mkamilifu.<br>• Sisi vilevile, hatumtii Mungu na tunahitaji kuhuzunika juu ya zambi zetu na kumuomba atusamehe.<br><br>**Mstari muhimu:** ***ao Waroma 5:12, ao Waroma 5:1***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 3:1-24*** |
| KUTANGULIZA | • Onyesha picha nzuri, kisha kuiharibu kwa kuipasua ao kuipondaponda.<br>• Zungumza kuhusu hiyo. Nini inafikia picha? Inaonekana je sasa?<br>• Kueleza kwamba Mungu aliumba dunia kamilifu, lakini iliharibiwa. |
| KUFUNDISHA | • Wakati dunia ilipoumbwa hapo mwanzo, yote ilikuwa kamilifu. Lakini siku moja adui wa Mungu, Shetani, alijigeuza kama nyoka, aliingia katika bustani. Nyoka alimwambia Eva, akisema kwamba kama akikula tunda ya “mti wa kujua uziri na ubaya”, atakuwa pia na akili sawa Mungu. ***(Mwanzo 3:1-5)***<br>• Eva alimsikia adui wa Mungu. Kisha, alikosa kumtii Mungu kwa kuchukua tunda hiyo. Alimpa Adamu na walikula wote wawili. ***(Mwanzo 3:6)***<br>• Mangaribi hiyo, Mungu alitaka kuzungumza na Adamu na eva lakini walijua kwamba hawakutii na walijificha. ***(Mwanzo 3:7-8)*** *Ile imekwisha kukufikia kutokutii mtu? Kuna kitu kilifanyika baadaye? Eleza kwamba Adamu na Eva hawakuweza kufichama mbele ya Mungu, na sisi vilevile.*<br>• Mungu akaita: “Wewe ni wapi?” Alijua kwamba Adamu na Eva hawakutii, na hata kama alikuwa angali anawapenda, alipaswa kuwaazibu sababu ya kutokutii kwao. Mungu aliwafukuza inje ya bustani. Zambi yao iliharibu uumbaji wa Mungu na kuharibu urafiki wao naye. Sababu ya zambi ya Adamu na Eva, dunia ilianza kutoa miiba na michongoma. Wanyama na wanadamu walianza kugonjwa, na tena kibaya Zaidi, kifo kiliingia katika dunia. ***(Mwanzo 3: 9-24)***<br>• *Mungu pia anahuzunika wakati tunafanya ubaya. Mufikili pamoja kuhusu vitu ambavyo watoto wanaweza kufanya visivyopendeza Mungu. Ingawa ile, anatupenda. Yesu, Mwana wa Mungu, alikufa msalabani ili tusamehewe na kuwa marafiki za Mungu wakati tunatia tumaini letu ndani yake.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| KUJIFUNZA | Kujifunza mstari muhimu, ***Mwanzo 5: 12, ao Waroma 5:1***. Kueleza maana yake ikiwa ni lazima. |
| KURUDIA | • Ni nani aliyemujaribu Eva kwa kumuonyesha achukue tunda?<br>• Jinsi gani shetani alimvuta Eva achukue tunda?<br>• Eva alimpa nani tunda?<br>• Adamu na Eva walifanya nini wakati Mungu alipowaita?<br>• Mungu alipata wazo gani kulingana na zambi ya Adamu na Eva?<br>• Ni nini iliwapata Adamu na Eva?<br>• Mungu anawaza nini wakati tunafanya ubaya?<br>• Namna gani tunaweza kusamehewa makosa tunayoyatenda? |

# A2 SOMO 1
## Noa anamtii Mungu

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Noa, familia yake na wanyama walikingwa ndani ya safina.<br>• Mungu anatupatia njia ya wokovu wetu na tunaweza kumtumainia kama vile Noa alifanya.<br><br>**Mstari muhimu:** ***ao Matendo 16:31***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 6:5-25*** |
| **KUTANGULIZA** | • Uwaulize watoto waseme ni wanyama gani wanapenda.<br>• Waza kwamba wanyama hawa wote weko pamoja! Ni fasi gani tungeweza kuwaweka wote? Tungesikia makelele gani? tungenusa harufu gani?<br>• Eleza kwamba watajifunza historia moja ya Biblia ambamo watu wamoja na wanyama wengi walipanda ndani ya safina kubwa. |
| **KUFUNDISHA** | • Katika mwanzo, wakati Mungu alipoumba dunia, vyote vilikuwa vizuri na vya kupendeza. Lakini baada ya muda mfupi, Adamu na Eva hawakumtii Mungu. Watoto wao wamekuwa wenye ubinafsi pia wabaya na Mungu alijuta kwa nini aliwaumba. ***(Mwanzo 6:5-6)***<br>• Dunia yote ilikuwa mbaya sana lakini mtu mmoja alibaki akimpendeza Mungu! Aliitwa Noa. Mtu huyu na mke wake, na wana wao watatu na wa bibi zao, walijaribu kufanya kila kitu ambacho Mungu alitaka, lakini ma familia ingine yote kandokando yao walikuwa wanajiwazia mpaka wao wenyewe na walimwacha Mungu kabisa. ***(Mwanzo 6:8-10)***<br>• Mungu aliamua kuazibu dunia yote, kwa maana ilikuwa mbaya. Alitaka kwamba Noa afanye chombo kikubwa sana kinachoitwa safina. Wakati kitakapokuwa tayari, Mungu atatuma uharibifu kubwa, unaoitwa garika ya maji, juu ya kufunika inchi yote. Kwa hiyo, kila kitu ambacho kiliishi duniani kilipaswa kufa, ila tu Noa na familia yake, walikuwa salama ndani ya safina. ***(Mwanzo 6:7-18)***<br>• Noa alitii katika yote kwa kila kitu ambacho Mungu alimuomba. Kulikuwa lazima ya miaka karibu mia moja kwa kujenga hicho chombo kikubwa, safina. *Zungumzia ukubwa wake, kubwa kama uwanja wa mpira, ni yenye viwango tatu vya urefu juu.* Mwisho, kisha kazi mrefu sana na ya nguvu sana, safina ilimalizika ***(Mwanzo 6: 25)***<br>• Mungu alimwambia Noa aingize ndani ya safina wanyama na ndege za aina zote. *Taja wanyama kati ya wale ambao walitajwa na watoto katika utangulizi.* Hawa watakuwa salama pamoja na Noa na familia yake. *Fanyeni pamoja hesabu ya wa memba mnane wa familia yay a Noa ambao waliingia katika safina.* Wakati wote walipokuwa ndani, Mungu alifunga mlango. Mpango wake juu ya wokovu wao ulitimizwa vizuri. ***(Mwanzo 7:13-16)***<br>• *Eleza kwamba sisi pia, tunatenda mambo mengi mbaya. Tunahitaji kuokolewa kwa azabu ambayo zambi zetu zimestahili. Mungu anatupatia njia ya wokovu, kwa kutia tumaini letu ndani ya Mwana wake, Bwana Yesu. Yeye ni kama safina ambayo Mungu alitayarisha kwa ajili yetu.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Matendo 16:31***. Kueleza maana yake ikiwa ni lazima. |
| **KURUDIA** | • Kulikuwa jambo gani katika dunia?<br>• Mungu aliamua kufanya nini?<br>• Ni nani ambaye alimpendeza Mungu?<br>• Mungu alimuomba Noa afanye nini?<br>• Ni nani aliingia katika safina?<br>• Ni nani ambaye alifunga mlango wa safina?<br>• Kwa nini watu walio katika safina walikuwa katka salama?<br>• Namna gani tunaweza kuokolewa kwa azabu sababu ya zambi zetu? |

## A2 SOMO 2
**Katika salama ndani ya safina**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Noa na familia yake walikuwa walikuwa walilindwa kwa sababu walimtumaini Mungu na kumtii.<br>• Mungu alliahidi kutulinda ikiwa tunamtumaini.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Mezali 29:25***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 7:1-16*** |
| **KUTANGULIZA** | • Uwaambie watoto wazungumzie kuhusu kitu ambacho walijenga ao kukitengeneza. Ulitumia nini kwa kukifanya? Ilikuwa mwepesi? Kuna mtu ambaye alikusaidia?<br>• Kurudia historia iliyopita. Noa alitumia nini kwa kujenga safina? Unawaza kwamba ilikuwa magumu kwa kutimiza ? Aliifanya kwa sababu ya nini ?<br>• Uwakumbushe kwamba hata kama ilikuwa kazi ya magumu, Noa aliifanya kwa sababu Mungu alimwambia. Alitii kabisa maagizo ya Mungu. |
| **KUFUNDISHA** | • Noa na familia yake walikuwa salama katika safina. ***(Mwanzo 7:6-7)***<br>• Baada ya siku saba, mvua ilianza kunyesha. Na mvua iliendelea kunyesha, siku kwa siku! Majani yote na mauwa yote vilifunikwa na maji. Mito na bahari vilijaa na kusababisha uharibifu kubwa. ***(Mwanzo 7:17-20)***. *Eleza kwamba sasa wakati ilikuwa imekwisha kupita sana kwa watu wote ambao walikuwa wakimzihaki Noa, na ambao sasa walikuwa inje ya safina.*<br>• Maji iliendelea kupanda juu sana. Ilifika kufunika ma nyumba, miti, hata pia milima mirefu sana. ***(Mwanzo 7:20-21)*** *Jaribu kuwaza jinsi Noa na familia yake walikuwa katika safina. Ni nini ingefika ikiwa Noa hakumtii Mungu?*<br>• Ndani ya safina, Noa, familia yake na wanyama wote walikuwa salama! Kwa sababu Noa alitia tumaini lake ndani ya Mungu na alimtii, Mungu aliwalinda wote. ***(Mwanzo 7:23)***<br>• *Ambia watoto kwamba Mungu anataka kwamba sisi pia, tumutumainie na tumtii. Mungu aliahidi kutulinda sisi vilevile, ikiwa tunamtumainia na tunamtii, kama vile Noa.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Mezali 29:25***. Kueleza maana yake ikiwa ni lazima. |
| **KURUDIA** | • Noa alionyesha namna gani Imani yake kwa Mungu?<br>• Ni nani ambaye aliingia na noa katika safina?<br>• Walifanya siku ngapi ndani ya safina mbele ya mvua kwamza kunyesha?<br>• Maji ilipanda urefu gani?<br>• Ni nani ambaye alikuwa salama?<br>• Kwa nini Noa alilindwa?<br>• Ni nani ambaye atatulinda ikiwa tunatia tunamtumainia? |

## <u>A2 SOMO 3</u>
## Mwanzo mpya

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Mungu alimpa Noa na familia yake dunia mpya na safi.<br>• Mungu anaweza kufanya maisha yetu iwe mpya na safi kama tunamuomba atusamehe.<br><br>**Mstari muhimu:** ***2 Wakorinto 5:17***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 8:1-19*** |
| **KUTANGULIZA** | • Kueleza watoto kwamba Noa na familia yake walikaa muda mrefu ndani ya safina.<br>• Kuwatia watoto moyo wafikirie maisha ndani ya safina. Ungefanya nini mchana wote? Ungewaza nini kuhusu ile yote? Kwako wewe, ungejisikiaje? |
| **KUFUNDISHA** | • Baada ya siku makumi ine, mwishowe mvua ilimalizika. Lakini ilikuwa bado inafunika milima. ***(Mwanzo 8:1-4)***<br>• • Siku moja, Noa aliachilia kunguru kutoka safina, ili aone kama maji yalishuka. Ndege alikuwa anaenda na kurudi hata inchi ilipokauka. Baadaye, Noa aliachilia njiwa ambaye alirudi kwa haraka. Baada ya wiki moja, alimwachilia tena na wote walifurahi kwa kuona ndege amerudi na jani la mzeituni katika mdomo wake. *Eleza kwamba ile ilimaanisha kwamba juu ya milima ilikuwa sasa inje ya maji.* ***(Mwanzo 8:6-11)***<br>• Baada ya siku saba, Noa alitoa tena hua. Mara hii, hakurudi tena. Noa alijua kwamba kiwango cha maji kimeshuka na Noa alipata fasi ya kuishi. Mwishowe, safina ilisimama kwenye milima ya ararati. ***(Mwanzo 8:4 na 12)***<br>• Wakati inchi ilipokuwa tena kavu, Mungu akamwambia Noa atoke katika safina na wanyama wote. Habari njema gani kwa wote! *Kulingana na wewe, noa na familia yake walijisikiaje wakati mwishowe waliweza kutoka katika safina? Muzungumze na watoto kuhusu hiyo inchi mpya, jinsi ilivyokuwa.* ***(Mwanzo 8:15-19)***<br>• *Eleza kwamba sisi hatuna tofauti na watu wa siku za Noa. Lakini Mungu anaweza kuondoa vitu vibaya katika maisha yetu na kutupa moyo mpya na safi. Tunapaswa kuomba Mungu atusamehe na kumtumainia Bwana Yesu ambaye alikufa msalabani kwa ajili ya kuondosha zambi zetu.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***2 Wakorinto 5:17***. Kueleza maana yake ikiwa ni lazima. |
| **KURUDIA** | • Ni ndege gani ambaye noa alimtoa wa kwanza kutoka safina?<br>• Njiwa alileta nini katika mdomo yake mara ya pili?<br>• Safina ilisimama wapi?<br>• Ni nani alimwambia Noa atoke katika safina?<br>• Ni nani aliokolewa katika garika?<br>• Ni nani ambaye aliazibiwa sababu ya zambi zetu?<br>• Tunapaswa kufanya nini kwa kuwa na moyo safi?<br>• Jaza na maneno yanayokosa: “hivi kama mtu akiwa ndani ya Kristo, yeye ni ..... kipya. |

**A2 SOMO 4**
**Ahadi ya Mungu**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Kila mara Mungu anatimiza ahadi zake.<br>• Kama vile Mungu livyomtunza Noa na familia yake, aliahidi kwamba hatawaacha kamwe wale ambao wanamtumainia na kumufuata.<br><br>**Mstari muhimu:** ***ao Hesabu 10:29, ao Waebrania 13:5***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 8:1-19*** |
| KUTANGULIZA | • Uwaambie watoto mfano wa ahadi moja ambayo mtu fulani alifanya kwako.<br>• Acha watoto (katika vikundi vya wawili) wazungumzie ahadi moja ambayo ilifanywa kwao.<br>• Kuwauliza kama kuna mmoja ambaye amekwisha kufanya ahadi ile hakuweza kutimiza.<br>• Kuwaambia watoto kwamba katika Biblia muna ahadi nyingi za Mungu na kila mara anaitimiza yote!<br>• Eleza kwamba kama tunachagua kutia tumaini letu ndani ya Mungu na kumfuata, aliahidi kwamba hatatuacha kamwe. |
| KUFUNDISHA | • Noa na familia yake walikuwa salama! Walikaa muda mrefu katika safina, wakati Mungu aliwaonyesha kwamba wanaweza sasa kuondoka pamoja na wanyama wote. ***(Mwanzo 8:15-19)***<br>• Kitu cha kwanza ambacho Noa alitaka kufanya, ni kusema “aksanti” kwa Mungu kwa kuwa aliwalinda, yeye na familia yake, walikuwa salama wakati wa garika! Kwa hiyo, alikusanya mawe makubwa ambayo aliyaweka pamoja ili ajenge mazabahu. Siku za Noa, watu walikuwa wanachoma zabihu ya kuteketezwa ili kumshukuru Mungu kwa yote ambayo alifanya kwa ajili yao. ***(Mwanzo 8:20-21)*** Tunaweza kumshukuru Mungu sababu ya mambo gani? *(Unaweza kufanya daftari ya vitu juu ya hivyo unataka kusema aksanti kwa Mungu na kuandika katika kibao ao katika karatasi kubwa).*<br>• Hii ilimpendeza Mungu, kwamba Noa na familia yake wanawaza kumpigia aksanti. Sasa aliwafanyia ahadi ya ajabu:”sitalaani inchi tena kwa sababu ya mtu.” ***(Mwanzo 8:21-22)***<br>• Kisha akawaonyesha kile ambacho kitakuwa ukumbusho wa ahadi. Ilikuwa upinde wa mvua. Kila mara Noa na familia yake walikuwa wanaona upinde wa mvua, huu uliwakumbusha ahadi ya Mungu. ***(Mwanzo 9:12-13)*** *Zungumzia upinde wa mvua na rangi zake nzuri. Uwatie moyo watoto wafikirie kuhusu Mungu na ahadi zake kila mara wanapoona upinde wa mvua.*<br>• *Je, Mungu alitimiza ahadi yake kwa Noa? Saidia watoto kuelewa kwamba kila mara Mungu anatimiza ahadi yake ya kuwa nasi wakati tunatia tumaini letu ndani yake. (Tazama mstari muhimu wa pili).*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| KUJIFUNZA | Kujifunza mstari muhimu, ***ao Hesabu 10:29, ao Waebrania 13:5***, Kueleza maana yake ikiwa ni lazima. |
| KURUDIA | • Chagua kati ya maswali ya masomo iliyotangulia kuhusu Noa, ili uone ile watoto walikumbuka.<br>• Kurudia mistari muhimu ambayo watoto walishika katika walijifunza historia ya Noa.<br>• Watoto wanaweza kuchora sehemu ya historia wanayoipenda na/ao kuandika sentensi inayoeleza jambo ambalo wamejifunza.<br>• Kikundi moja ao darasa wanaweza kutengeneza picha za watu na wanyama wanaotoka katika safina, bila kusahau Mazabau na upinde wa mvua. |

## A3 SOMO 1
**Yesu anaita Petro**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Yesu alihitaji wasaidizi (wanafunzi) juu ya kutumika pamoja naye juu ya kuendeleza kazi yake.<br>• Kama tunataka kuwa wenye faida Yesu, ni lazima kumfuata na kumtii.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Matayo 4:19***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Matayo 4:18-22*** |
| **KUTANGULIZA** | • Muzungumzie pamoja kuhusu marafiki wale tunao. Ni wapi ulikutana mara ya kwanza na wale walio rafiki zako? Kwa nini ni kitu kizuri kuwa na marafiki? Ni tabia gani inaonekana kwa rafiki mwema? (Mapendekezo: upole wake, uaminifu wake, utayari wake wa kusaidia,...)<br>• Eleza kwamba Bwana Yesu alikuwa, yeye pia, na marafiki, na tutajifunza zaidi kuhusu wamoja wao.<br>• Tanguliza historia: Ziwa kubwa inayoitwa Galilaya yenye kuzungukwa na milima. Wavuvi weko wanafanya kazi pale. Eleza namna walikuwa wanafanya uvuvi wao (chombo, makila, na kazalika) ; ilikuwa kazi ya magumu! |
| **KUFUNDISHA** | • Yesu anaita Petro na ndugu yake Anderea. ***(Matayo 4:18-19)*** Petro na Anderea walikuwa wamekwisha kukutana na Yesu mbele na walijua kwamba alikuwa mtu wa muhimu kabisa. Sasa, Yesu anawaomba waache chombo chao cha uvuvi ili wajiunge kwake na kumsaidia katika kazi yake! *Tumia maneno ambayo Yesu alitumia na eleza kwamba kazi yao mupya itakuwa ya kuleta watu wengine wamjue Yesu. Kazi gani ya ajabu!*<br>• *Jibu ya Petro na Anderea.* ***(Matayo 4:20)*** pale pale walitambua kwamba ndio kitu kizuri kufanya. Walionyesha utayari wao kwa kwenda na Yesu pale pale. *Uilinganishe na jambo moja katika maisha ya watoto pale wanatii haraka. Muzungumzie pamoja kuhusu ile Petro na Andrea waliweza kusikia (mshangao, furaha, kujua kwamba walipendwa kwa sababu Yesu aliwachagua). Kwa wale wa kiwango cha 2, uwaambie kwamba wao sasa ni wanafunzi wa Yesu. Ile inamaanisha kwamba walikuwa tayari kwa kumfuata pahali popote atakapoenda, kwa kujifunza kwake, na kwa kumtii.*<br>• Yesu anaita Yakobo na Yoane. ***(Matayo 4:21-22)*** Baadaye siku hiyo hiyo, Yesu aliita tena wavuvi wengine wawili na wao pia walimfuata pale pale. (Kiwango 2)<br>• *Bwana anataka kwamba kila mmoja wetu awe mwanafunzi wake. Kama sisi ni wanafunzi wa Yesu, anaweza kututumia kwa kazi yake. Sawa vile wavuvi katika historia ya biblia, tunapaswa kutii Neno lake. Ni wapi tunakuta maneno yake imeandikwa? (Eleza umuhimu wa Biblia).*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Matayo 4:19***. Kueleza maana yake ikiwa ni lazima. |
| **KURUDIA** | • Wavuvi ambao waliitwa na Yesu ni ngapi?<br>• Walikuwa wanafanya kazi wapi?<br>• Ndugu wa Anderea alikuwa nani?<br>• Kulingana na ahadi ya Yesu, watakuwa je?<br>• Petro na Anderea waliacha nini nyuma yao wakati walienda na Yesu?<br>• Petro na Anderea walionyesha namna gani utayari wao wa kuwa wanafunzi wa Yesu?<br>• Wale wa ndugu wengine wawili ambao walihalikwa na Yesu walikuwa wa nani?<br>• Yakobo na Yoane walikuwa wanafanya nini wakati Yesu alipokuja?<br>• Ni nani alikuwa pamoja nao katika chombo?<br>• Jaza sentensi hiyo: Ikiwa tunataka kuwa wanafunzi wa Yesu, tunapaswa .......... Neno lake. |

## A3 SOMO 2
## Yesu anamsaidia Petro

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Nguvu ya Yesu ilitenda katika maisha ya Petro.<br>• Yesu ni Mwana wa Mungu, na anataka tumfuate, sawa vile Petro.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Luka 5:10***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Luka 5:1-11*** |
| **KUTANGULIZA** | • Uwaombe watoto wafikirie vitu ambavyo wanajua kufanya muzuri. Kuwakumbusha kwamba sisi wote tuko na uwezo wa kufanya kitu fulani, na kwamba kila mmoja wetu eko na uwezaji.<br>• Petro alikuwa na ujuzi wa uvuvi. Kulikuwa muda mrefu tangu alipokuwa mvuvi. Lakini katika historia ya leo, anajua kwamba ili kupata mafanikio ya kweli, inapaswa kumtii Yesu! (Itakuwa ya faida kwamba Petro aitwe pia Simoni ao Simoni Petro). |
| **KUFUNDISHA** | • Kumbusha watoto mazingira ya historia iliyo katika mafundisho iliyotangulia. Katika historia ya leo, Yesu anatumia chombo cha Petro na anafundisha watu Neno la Mungu. ***(Luka 5:1-3)***<br>• Agizo ya Yesu kwa Petro. Yesu alimwambia aingie katika maji mrefu zaidi na atupe pale nyavu ili avue samaki. ***(Luka 5:4-5)*** *Muzungumzie pamoja kuhusu ile Petro anawaza kwa jambo hili.*<br>• Uvuvi wa miujiza ***(Luka 5:6-7)*** *Unaonyesha tofauti na uvuvi wa usiku uliotangulia.* Ilikuwa ni muujiza! Yule ambaye aliumba samaki alikuwa pale, katika chombo pamoja na Petro, na ilikuwa uwezo wake ndio ulileta samaki katika nyavu.<br>• Jibu ya Petro. ***(Luka 5:10)*** Eleza kwamba Petro alielewa, mu namna mupya, Yesu ni nani kweli. Siye mtu wa kawaida sawa yeye. Yeye ni Bwana Yesu mwenye uwezo wote, na Petro alitambua kwamba, mbele yake, yeye ni mwenye zambi tu.<br>• Kazi mupya ya Petro. ***(Luka 5:10)*** Yesu akamwambia Petro kwamba tangu sasa atakuwa mvuvi wa watu! *Chunguza kama watoto wanaelewa wazo hii ambayo ilizungumziwa katika somo iliyotangulia.* Petro anajua sasa kwamba Bwana Yesu anampatia kazi ya muhimu zaidi, kwa hiyo aliacha yote ili amfuate. ***(Luka 5:11)***<br>• *Bwana Yesu anataka sisi tutambue ukubwa wake na nguvu yake. Tunaweza kuwa naye karibu. Yesu atabadilisha maisha yetu ikiwa tunachagua kumtii na kumfuata kama vile Petro alifanya.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Luka 5:10***. Kueleza maana yake ikiwa ni lazima. |
| **KURUDIA** | • Ni kitu gani Yesu alitumia ambacho kilikuwa cha Petro?<br>• Yesu anamwambia Petro afanye nini wakati alipomaliza kusema kwa makutano?<br>• Ni wakati gani Petro alivua samaki mara ya mwisho?<br>• Petro alifanya namna gani ili avue samaki nyingi?<br>• Ni jina gani ilipewa ku ile tendo kubwa Yesu alifanya, ambayo inaonyesha kwamba yeye ni Mwana wa Mungu?<br>• Sababu ya nini Petro alianguka kwenye miguu ya Yesu?<br>• Ni nani mwingine aliogopa sababu ya uvuvi wa miujiza?<br>• Yesu anamwambia Petro kwamba tangu sasa atafanya kazi ingine. Ni kazi gani?<br>• Petro na rafiki zake walifanya nini katika mwisho wa historia?<br><br>**Mapendekezo ya matendo:** Ikiwa una penseli, karatasi na mkasi, kila mtoto anaweza kuchora samaki na kumkatakata. Kisha, panga samaki zote pamoja na tangazo moja juu ya kukumbusha historia kwa watoto, kwa mfano: “Bwana Yesu alimsaidia Petro kukamata samaki nyingi”. |

**A3 SOMO 3**
**Yesu anatuliza zoruba**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Yesu aliweza kutuliza zoruba sababu alikuwa Mwana wa Mungu<br>• Tunapaswa kumwamini Bwana Yesu, Mwana wa Mungu.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Matayo 8:27***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Matayo 8:23-27*** |
| **KUTANGULIZA** | • Muzungumzie hali ya hewa katika eneo lenu. Je, inafika kwamba hali ya hewa inabadilika kwa ghafla, kwa mfano mvua inanyesha pasipo kutabiriwa?<br>• Muzungumzie hii jambo ya hali ya hewa kulingana na merikebu, hasa zaidi jinsi tendo ambayo upepo kubwa unafanya. Katika historia ya leo Yesu na wanafunzi wake wanavuka ziwa la Galilaya. |
| **KUFUNDISHA** | • Mwanzo wa kuvuka katika utulivu. Eleza jambo la wakati walipovuka na Amani; kwa wakati kidogo, Yesu amelala. ***(Matayo 8:23-24)***<br>• Zoruba. Kwa ghafla, zoruba kubwa imeamka na wanafunzi wameogopa. ***(Matayo 8:24)*** Eleza jambo hili kwa uwazi: Kelele, mawimbi inayoingia ndani ya chombo, kujikaza kuondosha maji inayoingia ndani ya chombo,...<br>• Woga wa wanafunzi. Eleza kwamba wameogopa sababu wanazani kwamba wao ni karibu kuzama. Kwa haraka, wanamwamsha Yesu na wanamsihi awaokoe. *Tumia maneno yao wenyewe.* ***(Matayo 8:25)*** Yesu anakata tamaa kwa kuona kwamba wanafunzi hawakuweza kumwamini. *Eleza kwamba "kuwa na imani" maana yake ni "kutumainia".* ***(Matayo 8:26a)***<br>• Mshangao wa wanafunzi. ***(Matayo 8 : 27)*** *Eleza kwamba wakati waliona nguvu ya Yesu ikitenda katika upepo na mawimbi, walitambua kwamba alikuwa tofauti nao.*<br>• Nguvu ya Yesu. Kisha, Yesu anasimamisha zoruba. ***(Matayo 8:26b)*** Angalia pia ***Marko 4:39***. *Kumbusha jambo la kwamba zoruba ilisimamishwa kabisa!*<br>• *Hakikisha kwamba watoto wanaelewa kwa nini Yesu aliweza kutuliza zoruba. Yeye ni Mwana wa Mungu ambaye aliumba kila kitu.*<br>• *Nguvu kamili juu ya kila kitu kilicho katika ulimwengu wetu, pia hali ya hewa. Uwatie moyo watoto wafikirie mambo ya maisha yao ambamo wanaweza kutia tumaini lao ndani ya Yesu, wakitambua kwamba kila mara yeye anatawala kila kitu.*<br>• *Imetupaswa kuamini kwamba yeye ni Mwana wa Mungu kweli.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Matayo 8:27***. Kueleza maana yake ikiwa ni lazima. |
| **KURUDIA** | • Historia hii inafanyika wapi?<br>• Ni nani ambaye alipanda wakwanza ndani ya chombo?<br>• Mawimbi yalifanya nini wakati zoruba ilipoanza?<br>• Yesu alikuwa anafanya nini wakati ule?<br>• Kwa nini wanafunzi walimwamsha Yesu?<br>• Kwa nini Yesu alikatishwa tamaa nao?<br>• Yesu alisimamisha vitu viwili, ni vitu gani?<br>• Mstari muhimu uko wapi katika Biblia?<br>• Kwa nini Yesu aliweza kutuliza zoruba, pale wanafunzi wake hawakuweza ?<br>• Ni jina gani ilipewa ku ile tendo kubwa ambayo Yesu alifanya ?<br><br>**Mapendekezo ya matendo:** Historia hii inaeleweka wepesi kwa njia ya mchezo kidogo, na wanafunzi 12 wenye kukaa katika chombo; watoto wengine wanaweza kufanya kelele za zoruba. Mtu mzima anaweza kusoma andiko la Biblia wakati watoto wanajipanga kwa kufanya michezo na kusema maneno yenye kufaa. |

## A3 SOMO 4
**Yesu anaokoa Petro**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Yesu alimwokoa Petro kwa kujibu maombi yake mfupi<br>• Tunapaswsa kutia tumaini letu ndani ya Bwana Yesu ili tuokolewe. .<br><br>**Mstari muhimu:** ***Matayo 14:33***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Matayo 14:23-33*** |
| **KUTANGULIZA** | • Eleza kwamba ni kwa kuishi pamoja na mtu ndipo unamjua Zaidi. Saidia Watoto wakumbuke kile Petro amejifunza kuhusu Yesu kufikia sasa.<br>• Acha watoto walete mawazo yao; ikiwezekana, andika katika kibao, kwa mfano: Yesu ni Mwana wa Mungu, anaweza kufanya miujiza, yeye eko na mamlaka juu ya bahari...<br>• Katika historia ya leo, Petro alijifunza tena kitu kipya kuhusu Yesu. |
| **KUFUNDISHA** | • Wanafunzi walienda katika chombo wakati Yesu alipoenda kuomba pekee. ***(Matayo 14:22-23)*** *Eleza umuhimu wa maombi katika maisha ya Yesu.*<br>• Upepo. ***(Matayo 14:24)*** *Kumbusha upepo wa historia ya wiki iliyopita na uifafanue.* Yesu anaona kwamba wanafunzi weko katika magumu, sasa anatembea kwenda kukutana nao katika ziwa, katikati ya usiku. ***(Matayo 14:25-27)*** *Ueleze ile wanafunzi waliwaza na jinsi walijisikia. Kumbusha misemo ya Yesu ya kutia moyo.*<br>• Ombi ya Petro. Petro anataka kuhakikishwa kwamba hakika ni Yesu na anamwambia amwite yeye pia kutembea juu ya maji! Yesu akasema: Kuja. Petro akashuka chomboni, akatembea juu ya maji ili aende kukutana na Yesu. ***(Matayo 14:28-29)*** Kila kitu kilikuwa sawa mpaka Petro alipoacha kumtazama Yesu na anaona mawimbi kubwa kandokando yake, anaanza kuzama!<br>• Yesu anaokoa Petro. T*umia maneno ya Petro ili ueleze jinsi alipaza sauti kwa Yesu mara moja ili amwokoe.* ***(Matayo 14:30-32)*** Kisha, wote wawili walipanda katika chombo na upepo ulitulia. *Ueleze jibu ya wanafunzi.* ***(Matayo 14:33)***<br>• *Petro, alihitaji kuokolewa katika kuzama. Tunahitaji kuokolewa katika zambi maishani mwetu. Peke yake tu Bwana Yesu anaweza kufanya ile kwa ajili yetu. Yesu alichukua azabu ambayo zambi yetu ilistahili kwa kufa msalabani. Imetupaswa kutia tumaini letu ndani yake.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Matayo 14:33***. Ueleze maana ya “kuinama”. Wanafunzi walishangaa sana na kupata furaha tele juu ya ile wanajifunza sasa kuhusu Yesu. Ueleze kwamba, pahali pote duniani, watu wanampenda Bwana Yesu na wanaweza, wao pia, kusema namna moja kama vile wanafunzi. |
| **KURUDIA** | • Maswali inaweza kutegemea masomo ine ya A3. Ikiwa uko na karatasi, unaweza kuchora samaki za fomu nyingi na urefu, na kuibandika; wakati mtoto anajibu swali, anachagua ao kukamata samaki mmoja kati ya hawa. Kwenye kila samaki imeandikwa kiwango fulani cha nukta. Watoto wanaunda timu mbili ambayo inaandika ma nukta wanayopata.<br>• Historia hizi zote zilifanyika wapi?<br>• Ongeza maneno inayokosekana katika shairi hii: “Unifuate na...”<br>• Yesu alimwambia nani maneno haya?<br>• Petro alifanya nini kwa kuona muujiza wa uvuvi?<br>• Ongeza maneno inayokosekana katika shairi hii “Ni mtu wa namna gani?...”<br>• Kwa nini Yesu alipanda mlimani?<br>• Ni kitu gani iliogopesha kabisa wanafunzi?<br>• Petro alijifunza nini kuhusu Yesu katika somo hii? |

## A4 SOMO 1
**Petro analala**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Maombi ilikuwa ya muhimu sana kwa Bwana Yesu.<br>• Ni ya muhimu pia kwetu sisi kuomba<br><br>**Mstari muhimu:** ***Yoane 15:14***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Matayo 26:36-46*** |
| **KUTANGULIZA** | • Zungumza mambo ambayo inaonekana kuwa magumu kwa watoto, kwa mfano kupiga mbio katika sehemu ya mwisho ya mbio, kuwa msikilivu kwa muda mrefu, ao tena kuwa mwenye kuangalia kwa muda Fulani wa ibada wakati saa imekwisha kupita kabisa.<br>• Katika mafundisho ya leo, Yesu anahitaji msaada wote wa rafiki yake Petro. Tutaona kama Petro alitenda kulingana na ile Yesu alitarajia kwake. |
| **KUFUNDISHA** | • *Eleza mazingira ya historia hii.* Yesu anajua kwamba wakati ambao atakufa msalabani umekaribia ili aakufe msalabani. Amekwisha kula chakula chake cha mwisho na wanafunzi wake. Mara kwa mara, Yesu alikuwa akimwomba Baba yake, na anajua mu kiwango gani ni ya muhimu kabisa kuomba wakati huu, juu ya ile inamuongojea. Alienda na wanafunzi wake katika shamba kule alikuwa na zowezo ya kwenda kuomba. Usiku ule, alitaka kwamba rafiki zake watatu Petro, Yakobo na Yoane, wakeshe na kuomba pembeni yake.<br>• Yesu aliwaambia Petro, Yakobo na Yoane wakeshe na waombe. ***(Matayo 26:36-38)*** Kisha alienda mbele kidogo na aliomba kwa Baba yake. *Eleza mambo ambayo Yesu aliyaishi ule muda. Maombi yake ilishuhudia kutaka kwake kumpendeza Baba yake katika kila kitu.* ***(Matayo 26:38-39)*** Baada ya saa moja, alikuta Petro na wengine wamelala. *Sema juu ya kukatwa tamaa kwa Yesu.* ***(Matayo 26:40-41)***<br>• Yesu alienda kuomba mara ya pili na alikuta rafiki zake wamelala tena ***(Matayo 26:42-43)***<br>• Aliomba mara ya tatu na wakati alipokuja tena kwao, waliendelea kulala. *Muzungumzie pamoja jambo la kwamba Petro na wengine hawakumsaidie Yesu. Pia hawakuweza kujiombea wao wenyewe katika wakati wa magumu huu mule walihitaji kabisa msaada.* ***(Matayo 26:44-45)***<br>• Ni wakati huo adui za Yesu walifika kwa kumkamata. ***(Matayo 26:45b-46)***<br>• *Kwa kumaliza, muzungumzie kuhusu umuhimu wa maombi kwetu. Inatusaidia kupata nguvu ndani ya Mungu na kushinda majaribu. Eleza mifano kidogo iliyo karibu na mambo ambayo watoto wanayoishi.*<br>• *Petro na wengine hawakutii agizo ya Yesu: “Mukeshe na kuomba”, lakini yesu anataka kwamba sisi tutii amri zake.*<br>• Kama wanafunzi hawakuweza kumsaidia Yesu, yeye kwa tofauti hakutuache. Aliomba na alipata nguvu ya kwenda mpaka msalabani ili atoe uzima wake kwa ajili yetu.<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Yoane 15:14***. Saidia watoto waelewe bahati walio nayo ya kuitwa rafiki za Yesu. |
| **KURUDIA** | • Yesu alienda kuomba wapi?<br>• Ni wanafunzi gani ambao walipaswa kuomba naye?<br>• Yesu aliomba neno gani?<br>• Yesu alijisikia je wakati aliipoomba?<br>• Ni ma saa ngapi Yesu aliomba mara ya kwanza?<br>• Kwa nini wanafunzi hawakuweza kuomba<br>• Mara ngapi Yesu aliwaambia waombe?<br>• Ni nini ilifanyika wakati Yesu alipomaliza kuomba?<br>• Msatri muhimu uko katika sura gani?<br>• Yesu anatuita wa nani kama tunamtii? |

## A4 SOMO 2
### Petro anapigana

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Yesu alijiacha kukamatwa na kuuawa kwa ajili yetu.<br>• Tunaweza kutuliza hasira yetu wakati tunajikuta katika magumu.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Waefeso 4:26***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Matayo 26:47-56*** |
| **KUTANGULIZA** | • Kurudia katika somo iliyotangulia na ile ilifanyika katika shamba. Petro na rafiki zake hawakuomba vile Yesu aliwaambia. Na sasa, watajikuta katika magumu zaidi. Watafanya nini? |
| **KUFUNDISHA** | • Eleza mazingira ya tukio hii. Kuna giza na kimya kabisa pahali pote…, lakini kwa ghafla, wanasikia nyayo nzito za askari wanaokaribia, wana silaha mikononi mwao. Petro na rafiki zake walijisikia je wakati ule?<br>• Kwa ghafla, Yuda anatoka katika kundi hii ya waadui. Amemkaribia Yesu na anambusu. *Eleza Yuda alikuwa nani na ni namna hii alipaswa kutambulisha wa askari Yesu ni nani. Eleza maana ya neno "usaliti". (Ona somo ya wakati wa biblia hatua ya 2)* ***(Matayo 26:47-50)***<br>• Wakati Petro alipotambua kwamba wa askari wanakuja kumkamata Yesu, anakasirika na anajaribu kumtetea Yesu kwa njia ya kushambulia mtu mmoja ambaye alikuwa katika kundi. ***(Matayo 26:51)*** *Ni kyepesi kwetu kukasirika na kutenda kama Petro. Sema mambo moja ao mbili ambamo watoto wanaweza kukasirika wepesi.* Kwa haraka, Yesu anamwambia Petro kurudisha upanga wake. *Eleza kwamba Yesu hakuhitaji kukingwa na Petro kwa sababu alijua kwamba yote ambayo ilitukia, ilikuwa katika mategenezo ya Mungu. Yesu alikuwa tayari kwa kujiacha akamatwe na kuuawa na adui zake. Alikuwa tayari kwenda hadi mwisho kwa ajili yetu. Onyesha tofauti iliyo kati kutenda kwa Yesu na kwa Petro.* Akikwisha kutoa yote kwa Baba yake, Yesu ni mtulivu. Lakini, Petro, ambaye asikuombe, asitende kamwe jinsi Yesu alitaka. ***(Matayo 26:52-56)***<br>• Wanafunzi waliogopa wanamwacha Yesu na wanakimbia. *Zungumza kuhusu ma sababu ambayo iliwasukuma kufanya hivyo.* ***(Matayo 26:56b)*** Petro pekee ndiye alijaribu kumfuata Yesu, kwa mbali, akiogopa yeye pia kukamatwa! *Saidia watoto kuwaza namna Petro alifanya ili asitambuliwe.* ***(Matayo 26:58)***<br>• *Eleza kwamba kama sisi ni wa Bwana Yesu, tunaweza kuomba, na kumuomba msaada wake ili tusikasirike, lakini ili atutulize. Roho Mtakatifu anayeishi ndani ya kila mukristo anatuwezesha kuwa na mwenendo muzuri.*<br>• *Muzungumzie kuhusu jambo moja ambayo mwisho wake utakuwa tofauti kama tunatenda kwa kasirani ao kwa utulivu.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Waefeso 4:26***. Eleza kwamba ikiwa tunakasirika, tunapaswa kutulia kwa haraka! |
| **KURUDIA** | • Ni nani ambaye alikuja katika shamba pamoja na adui za Yesu?<br>• Yuda aliwaonyesha namna gani kwamba huyu ndiye Yesu?<br>• Petro alibeba nini wakati Yesu alikamatwa?<br>• Ni sehemu gani ya mwili wa mtu ambayo ilikatwa na Petro?<br>• Yesu alimwambia Petro afanye nini?<br>• Mukristo anaweza kushinda hasira namna gani?<br>• Wanafunzi walifanya nini wakati Yesu alipokamatwa?<br>• Ni nani ambaye alijaribu kumfuata Yesu kwa mbali?<br><br>**Maonyesho:** Walimu wanaweza kucheza mchezo moja ao mbili ambamo mtu mmoja anakasirika sawa vile katika historia hapo juu. |

**A4 SOMO 3**
**Petro anamkana Yesu**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Wakati mwingine sisi sio washujaa na tunaacha marafiki zetu.<br>• Wakati hatuna waaminifu kwa Bwana Yesu, yeye ni tayari kwa kutusamehe.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Zaburi 51:9***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Matayo 26:69-75*** |
| **KUTANGULIZA** | • Zungumzia kuhusu sauti; inatusaidia kutambua mtu. Kama watoto wamezoea kutumia simu, wanajua kwamba inawezekana kutambua mtu kabla ya yeye kujitambulisha. Zungumzia pia kuhusu tofauti ya namna ya kutamka na jinsi inabadilisha kusikiwa kwa sauti; unaweza pia kuleta mfano ambao unaonekana katika inchi yenu.<br>• Unganisha hiyo na mafundisho ya wiki iliyopita. Uwakumbushe watoto kukamatwa kwa Yesu na kukimbia kwa wanafunzi. Lakini Petro, anataka kujua nini itafanyika kwa Yesu baadaye. |
| **KUFUNDISHA** | • Petro alikwenda kwenye uwanja la kuhani mkuu ***(Matayo 26:69a)*** *Eleza kwamba uwanja ilikuwa inje ya nyumba. Ikiwezekana, semea kuhusu uwanja moja ulio katika jengo fulani ambayo inajuliwa na watoto. Eleza mazingira ya tukio hiyo: Usiku wa baridi, moto wa kuni, walinzi na watumishi ambao walikuwa pia pale.*<br>• Kijakazi mmoja anamtambua Petro na anawaambia wengine kwamba Petro alikuwa pamoja na Yesu. Petro anajibu kwamba hajui mambo anayoyasema. ***(Matayo 26:69b-70)*** *Uwakumbushe kwamba kwa kusema hivi, Petro alisema uwongo.* Hakika alikuwa pamoja na Yesu! *Muzungumze pamoja kuhusu ma sababu ambayo ilimsukuma Petro kusema uwongo.*<br>• Wakati Petro anaelekea mlangoni, kijakazi mwingine anamtambua, mara tena, Petro amesema kwamba hamjui Yesu. ***(Matayo 26:71-72)*** *Eleza neno “usaliti” kwa watoto wa Kiwango cha 2.*<br>• Baadaye, mtu mwingine amesikia kwamba Petro eko anasema sawa mmoja wa wanafunzi wa Yesu. (Petro alikuwa mzaliwa wa Galilaya, vile vile Yesu na wanafunzi wengine. *Patanisha jambo hili na sehemu ya KUTANGULIZA) Eleza jinsi Petro alikasirika na kuogopa, ni ile ilimsukuma kumkana Yesu kwa mara ya tatu.*<br>• Jogoo aliwika na Petro alikumbuka maneno ambayo Yesu alimwambia mbele. ***(Matayo 26:34)*** *Ueleze kwa nini Petro alivurugwa sana.* ***(Matayo26:74b-75)***<br>• *Onyesha kwamba Petro alifanya kosa, yeye hakuwa na ujasiri wa kusema kwamba yeye ni mwanafunzi wa Yesu na alisema uwongo. Inatufikia kwamba sisi wote tunafanya makosa.*<br>• *Inafika kwamba sisi pia tunamkana Yesu kwa njia ya ile tunasema na kufanya. Yeye ni tayari kutusamehe makosa ambayo tulifanya. Anaweza kuifanya sababu alikufa msalabani kwa ajili ya zambi zetu.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Zaburi 51:9***. Eleza kwamba shairi hii ni maombi. Tunasoma humo kwamba, wakati tunamuoma Bwana Yesu asamehe zambi zetu, ni kama alikuwa anatusafisha na kututakasa kikamilifu, na kutufanya weupe kama theluji! Ikiwa ni lazima, eleza theluji ni nini. |
| **KURUDIA** | • Petro alikuwa anaongojea wapi?<br>• Ni nani ambaye alizungumza na Petro mara ya kwanza?<br>• Mara ngapi Petro alisema kwamba hamjui Yesu?<br>• Kwa nini Petro alisema uwongo huu?<br>• Mara ngapi Petro alisikia jogoo amewika?<br>• Alikumbuka nini wakati alisikia jogoo?<br>• Kwa nini Petro alilia?<br>• Tunapaswa kufanya nini ikiwa tumemkana Bwana Yesu? |

## A4 SOMO 4
**Petro na Yesu wanazungumza pamoja**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Yesu anamwambia Petro amuonyeshe mapendo yake baada ya yeye kumkana<br>• Bwana yesu anataka sisi tumpende<br><br>**Mstari muhimu:** ***1 Yoane 4:19***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Yoane 21:1-19*** |
| **KUTANGULIZA** | • Uwaambie watoto wakumbuke ma historia ya kwanza ambayo walisikia kuhusu Petro. Alikuwa anafanya kazi gani wakati Yesu alimwita hapo mwanzo?<br>• Eleza kwamba mambo mengi yalifanyika wakati huo kwa Petro. Alikuwa kati ya marafiki za karibu wa Yesu, lakini baadaye alimkana. (Kumbusha masomo tatu ya mwisho).<br>• Baada ya muda kidogo, Yesu alikufa msalabani, lakini alifufuka. Mara mbili, Yesu alikutana na wanafunzi wake na kwa hiyo aliwaonyesha kwamba alikuwa hai kweli! Katika siku zilizofuata, Petro aliamua kutoka akafanye uvuvi. |
| **KUFUNDISHA** | • Wanafunzi walifanya uvuvi usiku wote, lakini hawakupata kitu! ***(Yoane 21:3)*** *Muzungumzie kuhusu namna walijisikia (kuchoka, njaaa, kukatwa tamaa).*<br>• *Waza jinsi mambo ilifanyika: Jua imetoka, mtu amesimama kwenye pwani. Eleza mazungumzo kati ya wanafunzi na huyu mgeni.* ***(Yoane 21:4-6a)***<br>• Wakati walitii maagizo ya mgeni huyu, walipata samaki nyingi (15b). Kwa ghafla, Yoane anaelewa kwamba mtu huyu anapaswa kuwa Yesu. Petro anafurahi sana na anaruka kwenye maji ili aende kukutana na Yesu. ***(Yoane 21:7-8)*** *Jaribu kuwaza chakula kwenye pwani na ukazishe kusemea neno ya kwamba ilikuwa ya kipekee na hawakutarajia kuwa pale, pamoja na Yesu.*<br>• Kisha chakula hii ya asubui, Yesu anazungumza na Petro. Mara tatu anamuuliza kama anampenda. ***(Yoane 21:15-19)*** *Eleza ni mu kiwango gani ile ilikuwa ya muhimu kwa Petro. Kwa hiyo Bwana Yesu anamwambia kwamba anamsamehe na eko na kazi ya kipekee. Katika kiwango cha 2, kulinganisha ile mara tatu ambayo Petro alimkana Yesu na mara tatu ambayo anamuonyesha mapendo yake.*<br>• *Uliza watoto kama wamempenda Bwana Yesu.*<br>• *Wangejibu je swali ambayo Yesu alimuuliza Petro ? Yesu anapenda kwamba kila mmoja wetu ampende na amtumikie.*<br>• *Mungu anatupenda na anaonyesha mapendo yake kwa kutuma Mwana wake ili atuokoe. Tunapaswa kumpenda vile vile.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***1 Yoane 4:19***. Eleza maana yake ikiwa ni lazima. |
| **KURUDIA** | • Petro na marafiki zake walitoka kufanya uvuvi kwa muda gani?<br>• Yesu anawaomba kutupa makila ngambo gani?<br>• Walikamata samaki ngapi?<br>• Ni nani ambaye alikuwa wa kwanza kutambua kwamba ni Yesu?<br>• Ni nani ambaye alitaka kuwa wa kwanza kukutana na Yesu?<br>• Petro alifanya nini kabla ya kuingia katika ziwa?<br>• Ni nani alitayarisha chakula?<br>• Walikula nini?<br>• Ni maswali gani Yesu alimuuliza Petro mara tatu?<br>• Msari kubwa uko wapi katika Biblia?<br><br>**Mapendekezo ya matendo:** mambo ingine ya historia hii inaweza kurudiwa na watoto, kwa mfano kwenda kufanya uvuvi, kutambua mgeni kwenye pwani, kuruga katika maji, kuchukua samaki, kuihesabu. Uwaze pia kuiga misemo kama kukatwa tamaa, kushangaa, furaha. Kwa nini hauwezi kusoma maandiko ya Biblia na kuacha watoto wakusindikize na alama na misemo kwa kuonyesha historia? |

## A5 SOMO 1
**Abramu anaondoka katika inchi yake – Mungu aanamwita Abramu**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Abramu anamtii Mungu wakati aliondoka kule Uri<br>• Tunapaswa kuonyesha Imani yetu kwa Mungu kwa njia ya kumtii.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Mezali 3:5***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 12:1-9*** |
| **KUTANGULIZA** | • Uzungumzie kuhama, ikiwa ile inafanana na kitu fulani ambacho watoto wanaweza kuelewa.<br>• Wanawaza nini kuhusu wazo ya kwenda katika inchi ingine, mbali sana na kwao? Watafurahi, watasikitika, watakuwa na huzuni, watakuwa wenye heri? Leta ma sababu.<br>• Umtambulishe Abram na ueleze maisha yake ilikuwa namna gani katika mji wa Uri: familia, marafiki, nyumba, wanyama, mali..., yote ambayo ilihitajiwa! |
| **KUFUNDISHA** | • Siku moja Mungu alimwambia Abramu: "Toka wewe katika inchi yako na uende katika inchi ambayo nitakuonyesha". ***(Mwanzo 12:1)*** *Ni nini ilikuwa kigumu katika ile Mungu alimwambia Abramu? (Kuacha maisha yake ya starehe nyumbani, kwenda bila kujua anaenda wapi).*<br>• Mungu alifanya ahadi kwa Abramu. ***(Mwanzo 12:2-3)*** *Eleza kwamba ahadi zote za Mungu zilielekea vitu vizuri, kwa mfano kuwa taifa kubwa na jina kubwa. Alitaka kumbariki Abramu. Wakati Mungu anabariki mtu, anamuonyesha wema wake.*<br>• Abramu alitii Mungu. ***(Mwanzo 12:4)*** *Kwa nini Abramu alitii? (Aliamini ahadi za Mungu, alimtumainia Mungu).*<br>• *Eleza ni wanani ambao walienda pamoja na Abramu: Mke wake sarai, mwipwa yake Loti, watumishi wake. Mungu pia alikuwa pale kwa kuonyesha njia. Eleza safari hiyo kwenye mgongo wa ngamia. Muda wa safari hii mrefu katika jangwa, walikuwa wanalala usiku ndani ya ma hema.*<br>• Mwisho abramu anafika inchi ya kanana. ***(Mwanzo 12:6-9)***<br>• *Abramu alijisikia je? Eleza kwamba kwa kujenga mazabahu, Abramu alionyesha shukrani yake kwa Mungu.*<br>• Taja mambo tofauti ambamo Mungu anapenda tumtumainie.<br>• *Onyesha kwamba ile inamaanisha imani kamili kwa Mungu ; kumtegemea ili mambo yote imalizike vizuri, kulingana na yeye, kuliko kutumainia mawazo na uwezji wetu sisi wenyewe.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Mezali 3:5*** Eleza kwamba mstari huu unaonyesha kwamba ile Abramu alifanya: Alimtumainia Mungu kwa moyo wake wote kuliko kutafuta njia zake yeye mwenyewe. |
| **KURUDIA** | Tumia ma sentensi ifwatayo ambayo kila mara jibu ni "ndio" ao "hapana" kwa ajili ya kukamilisha majifunzo ya somo hii.<br>• Mungu alizungumza na Abramu.<br>• Abram alitoka katika inchi yake sababu ya njaa.<br>• Mungu alilaka kumbariki Abramu.<br>• Abramu alikuwa na miaka 70 wakati alipoondoka katika inchi yake.<br>• Abram alijua kwenye alienda.<br>• Abram alikuwa na mtoto anayeitwa Loti.<br>• Mungu alimwongoza Abram kufika inchi ya Kanana.<br>• Katika hiyo inchi mpya, Abram aliishi ndani ya nyumba.<br>• Abramu alionyesha Imani yake kwa Mungu kwa kumtii.<br>• Mungu anataka kwamba tumtumainie na kumtii. |

## A5 SOMO 2
**Abramu na Loti**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Loti alichagua.<br>• Ni ya muhimu kwetu kufanya uchaguzi mzuri<br><br>**Mstari muhimu:** ***Wafilipi 4:19***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 13:1-18*** |
| **KUTANGULIZA** | • Muzungumzie uchaguzi ambao wana wa Israeli wanapaswa kufanya na uwezekano wa kuruhusu wengine kuchagua wa kwanza. Leta mfano moja ambao unapatana na utamaduni wako.<br>• Muzungumzie kuhusu mabishano na namna yanaharibu mahusiano. |
| **KUFUNDISHA** | • Watumishi wa Abramu na Loti walikuwa wakibishana kuhusu fasi ambapo kuna majani, kwa ajili ya kupeleka wa nyama wao kwa kuwalisha ***(Mwanzo 13:5-7)***.<br>• Abramu anajua kwamba mabishano ni kitu kibaya, kwa hiyo anamwambia Loti kwa kwa ukarimu achague wa kwanza malisho anayotaka kwa ajili ya wanyama wake. ***(Mwanzo 13:8-9)***<br>• *Eleza mazingira, ukionyesha wazi tofauti iliyo kati ya uwezekano wa kuchagua kwa Loti: Uwanja wa Yorodani ulio na maji mengi ambapo majani inakuwa kwa wingi, ao udongo usiozaa wenye kuzungukwa na ma bonde. Unawaza kwamba Loti atachagua nini?*<br>• Kuchagua kwa Loti. ***(Mwanzo 13:10-13)*** *Kwa nini Loti alifanya uchaguzi huu? (Aliona ile ambayo ilionekana kuwa mzuri na aliitaka iwe yake). Loti alikuwa mharibifu na mwenye ubinafsi, kama vile sisi pia tunaweza kuwa. Eleza kwamba kuchagua kwa Loti, ingawa vile kulionekana muzuri, kulikuwa kubaya, kwa sababu watu ambao walikuwa wanaishi kule hawakumpendeze Mungu hata kidogo.*<br>• Abramu na Loti waliachana, lakini Mungu alimuahidi Abramu kwamba siku moja, atampatia yeye na familia yake, inchi ambayo aliweza kuona kwa mbali ***(Mwanzo 13:14-18)***<br>• *Ungejisikia je ikiwa wewe ungekuwa Abramu? Ungejisikia kwamba umedanganywa? (Onyesha kwamba Abramu alikuwa na ahadi za Mungu ambayo ilikuwa na bei kabisa kuliko ile Loti alichagua).*<br>• *Loti alifanya uchaguzi mbaya. Tunapaswa kuchagua kwa hekima. Ya muzuri zaidi kuliko yote, ni kumwita Bwana Yesu Kristo aingie ndani yako ili asamehe zambi zako.*<br>• *Onyesha kwamba Mungu anajua kilicho kizuri zaidi kwetu na kwamba anaweza kujibu mahitaji yetu kikamilifu, kama vile aliweza kumpa Abramu yote ambayo alihitaji. Eleza kwamba Mungu ni mwaminifu; kila mara anatimiza ahadi zake.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***ao Mwanzo 15:13, ao Wafilipi 4:19***, ukiipatanisha na historia ambayo watoto wanasikia sasa hivi. |
| **KURUDIA** | Mwisho wa historia, Abramu alijenga mazabahu. Vikundi vinaweza kuundwa. Mtoto anayeleta jibu yenye kufaa kwa maswali ifwatayo, anaweza kutupa kura ili wingi fulani wa mawe kwa ajili ya kikundi chake. Mawe ya kweli, ao picha za mawe, inaweza kutumiwa. Kikundi ambacho kinawina ni kile kinapanga mawe mengi juu ya “mazabahu” yake.<br>• Tunajua namna gani kwamba Abramu alikuwa mtu tajiri?<br>• Ni nani aliamua kumaliza mabishanio?<br>• Ni nani ambaye alichagua wa kwanza?<br>• Loti aliona mtoni gani?<br>• Loti alienda upande gani?<br>• Ni nini haikuwe mzuri katika ile Loti alichagua?<br>• Mungu alimwabia Abramu aangalie upande gani?<br>• Mungu alifanya ahadi gani kwa Abramu? (Inchi na familia)<br>• Ni kwa heshima ya nani Abramu alijenga mazabahu?<br>• Ni uchaguzi gani wa muhimu tunapaswa kufanya katika maisha yetu? |

## A5 SOMO 3
## Ahadi za Mungu

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Kwa sababu Mungu anajua wakati ujao, anaweza kufanya ahadi kuhusu mambo itakayofanyika.<br>• Mungu anataka kwamba tuamini ahadi zake.<br><br>**Mstari muhimu:** ***ao 1 Wakorinto 10:13, ao Mwanzo 15:6***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 15:1-7*** |
| **KUTANGULIZA** | • Chagua mfano moja wa ahadi ambayo inaweza kufanywa kwa ajili ya watoto. Onyesha hali ya tumaini ile watakuwa nayo wakati wa kuongojea, pia furaha ya kutarajia kutimilika kwa ahadi hii. (Unaweza pia kuleta mfano wa ahadi ambayo juu ya sababu moja ao ingine haikutimizwe).<br>• Kama wanadamu, tunaweza kukosa kutimiza ahadi, hata kwa nia nzuri, lakini Mungu yeye, kila mara, yeye anatimiza ahadi! |
| **KUFUNDISHA** | • Mungu alizungumza na Abramu katika maono na alimwahidi mtoto mwanaume. ***(Mwanzo 15:1, 4)*** *Patanisha hii na ahadi ambayo alipewa mbele. Onyesha mu kiwango gani habari hii ni ya ajabu kwa Abramu, ambaye amekwisha kuwa na zaidi ya miaka 90!*<br>• Mungu alimuonyesha Abramu ma nyota. Alimwambia kwamba familia yake itakuwa nyingi kama nyota. ***(Mwanzo 15:5)*** *Muwaze pamoja na watoto ikiwa ni lazima kuhesabu nyota: Haiwezekane kamwe! Uwaache washangae mbele ya uwingi wa nyota na ukubwa wa muumbaji wake.*<br>• Abramu aliamini ahadi za Mungu. ***(Mwanzo 15:6)*** *Eleza ma sababu juu ya ile Abramu alimwamini Mungu.*<br>• Mungu alileta ma jina mpya kwa Abramu na Saraï, ***(Mwanzo 17:5, 15)*** *Jina mpya ya Abrahamu maana yake ni "baba ya mataifa mengi", ili kila mara akumbuke ahadi za Mungu*<br>• *Mungu alifanya ma ahadi kwetu katika Neno lake, Biblia. Leta mifano moja inayoelekea wale wanaomtumainia*<br>• *Inampendeza Mungu wakati tunaamini ile anasema.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***ao 1 Wakorinto 10:13*** ("Mungu ni mwaminifu"). Eleza kwamba neno "mwaminifu" inamaanisha kwamba tunaweza kumtumainia Mungu. Atatimiza ahadi zake. ***Ao Mwanzo 15:6***, Eleza kwamba ilimpendeza Mungu wakati Abramu alimtumainia. |
| **KURUDIA** | • Kulingana na ahadi ambayo imekwisha kupewa kwa Abramu, atakuwa baba wa nani?<br>• Ni ahadi gani Mungu alifanya kwa Abramu katika maono?<br>• Mke wa Abramu alikuwa nani?<br>• Mungu alimuonyesha Abramu nini?<br>• Mungu alilinganisha nyota na nini?<br>• Abramu alifanya nini wakati Mungu alimfanyia ahadi hii?<br>• Jina mpya ya Abramu ilikuwa nini<br>• Jina mpya ya Saraï ilikuwa nini?<br>• Mungu anataka tufanye nini wakati tunajua ahadi zake kwetu?<br>• Neno "kuamini" inamaanisha nini? |

## A5 SOMO 4
**Wageni kwa Abrahamu**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Mungu alichagua ma njia tofauti ili atume ujumbe zake kwa watu, zaidi kabla ya Biblia kuandikwa. Wageni watatu wa muhimu walileta kwa Abrahamu ujumbe kutoka kwa Mungu.<br>• Mungu ni mwaminifu kwa ile anaahidi. Hakuna kisichowezekana kwake.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Mwanzo 18:14***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 18:1-15*** |
| **KUTANGULIZA** | • Zungumza kuhusu mambo inayofanyika katika tamaduni yenu wakati watu wanafika bila kutarajiwa. Unaweza kutumia vitu fulani kwa kuonyesha ile kwa njia ya mchezo kuhusu kupokelea mgeni ambaye anafika bila kutarajiwa.<br>• Zungumza jinsi wageni walifika kwa Abramu. Anakaa kwenye mlango wa hema yake katika joto la jua. Anaona watu wanakaribia. “Wanaweza kuwa wa nani?” anajiuliza. |
| **KUFUNDISHA** | • Abrahamu amekaribisha watu na kuwatolea maji na chakula ***(Mwanzo 18:2-8)*** *Eleza kazi ya sara. Onyesha mambo yote vile ilifanyika: Jua kali, maji ya baridi kwenye miguu ya moto, harufu ya chakula.*<br>• Baada ya chakula, wageni hawa watatu wanamjulisha Abrahamu kuhusu Sara: Mwaka ujao atapata mtoto mwanaume. ***(Mwanzo 18:9 na 10)*** *Wageni walijua ile namna gani? Eleza kwamba watu hawa ni wajumbe kutoka mbingu, wanatumwa na Mungu. Mmoja kati ya hawa watatu ni Bwana Yesu, na wengine wawili ni wa malaika. Muzungumzie pamoja kuhusu vile Abrahamu alijisikia kwa kupata habari hii*. Ahadi za Mungu ni karibu kutimilika!<br>• Sara amecheka sababu kwake, ile inaonekana kwamba haiwezekane, lakini hakika Mungu analaka kufanya kisichowezekana! ***(Mwanzo 18:1-15)*** *Muzungumzie kuhusu jinsi Mungu aliweza kujisikia wakati Sara alicheka.*<br>• Baada ya mwaka moja, mtoto alizaliwa. ***(Mwanzo 21:1-7)*** *Jaribu kuwaza furaha ambayo walikuwa nayo. Mungu alitimiza ahadi yake? Kwa watoto wa kiwango cha 2, unaweza kueleza maana ya jina Isaka (“amecheka”).*<br>• *Tunaweza kumtumainia Mungu kuhusu ahadi zake zote kwetu. Hakuna kisichowezekana kwake. Habadilike! Ni Mungu gani wa ajabu na mwenye kustahili tumaini letu lote.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Mwanzo 18:14***. Eleza maana yake ikiwa ni lazima. |
| **KURUDIA** | Ma swali ifwatayo ni kulingana na historia hii. Unaweza kuitumia, ao kutunga ingine katika msururu wote wa masomo ine ya muundo wa A5.<br>• Ni wakati gani katika mchana watu hawa watatu walikuja?<br>• Abrahamu alikuwa wapi wakati ule?<br>• Abrahamu alimuomba Sara afanye nini?<br>• Walikula nini ingine?<br>• Sara alikuwa wapi wakati wajumbe walijulisha habari yao?<br>• Kwa nini Sara alicheka?<br>• Kulingana na ujumbe huu, Sara atapata mtoto wakati gani?<br>• Ni jina gani ilipewa kwa mtoto?<br>• Abrahamu alikuwa na miaka ngapi wakati wa kuzaliwa kwa Isaka<br>• Taja ma sababu mbili juu ya hiyo Abrahamu na sara walikuwa na furaha. (Walipata mtoto mwanaume, Mungu alitimiza ahadi yake).<br><br>**Maonyesho:** Watoto watapendezwa kwa kuona mchezo kuhusu sehemu ya kwanza ya historia hiyo. Onyesha wazi kila tendo. Watu wazima wanaweza kuiga Abrahamu, Sara, mtumishi na wageni watatu. Ao, katika vikundi kidogo, watoto wanaweza kufanya michezo, na misemo, kuiga watu. |

**A6 SOMO 1**
**Abrahamu anamsikia Mungu**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Abrahamu alimpenda Mungu zaidi ya yote<br>• Sisi pia, tunapaswa kumpenda Mungu kwa moyo wetu wote<br><br>**Mstari muhimu:** ***Mwanzo 22:8, ao Kumbukumbu la Torati 6:5***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 22:1-9*** |
| **KUTANGULIZA** | • Uwaulize watoto ni vitu gani ambavyo ni vya muhimu sana katika maisha yao. Kwa nini vitu hivi ni vyenye bei ku macho yao?<br>• Kisha kuwauliza wangefanya je ikiwa ni lazima kuacha vitu hivi? Wangetamani kufanya vile? Wangejisikia je? Eleza kwamba katika somo ya leo, Abrahamu anapaswa kuacha kitu Fulani (mtu fulani) ambacho kina bei kabisa kwake. |
| **KUFUNDISHA** | • Mungu alitimiza ahadi yake na aliwapa mtoto mwanaume, Abrahamu na Sara. Aliitwa Isaka. Wazazi wake walimpenda sana. ***(Mwanzo 21:1-3)***<br>• Siku moja, Mungu alimuomba Abrahamu alete Isaka katika inchi ya Morija. Inaonekana kwamba Isaka alikuwa angali kijana. Mungu anataka kwamba Abrahamu atoe mwana wake kama sadaka ya kuteketezwa. Mungu eko anamjaribu Abrahamu, ili aone mu kiwango gani anampenda. Hata kama hii ombi ya Mungu inamhuzunisha, Abrahamu anamtumainia Mungu na kumtii. ***(Mwanzo 22:1-2)*** *Abrahamu alimpenda Mungu kwa moyo wake wote. Alikuwa anamsikia Mungu na alikuwa tayari kwa kumtii hata wakati alimwomba kitu kigumu.*<br>• Asubui mapema, Abrahamu alitayarisha kila kitu kwa ajili ya safari. Alikata kuni juu ya sadaka ya kuteketezwa. Alichukua watumishi wawili na mwana punda. ***(Mwanzo 22:3)***<br>• Kisha kutembea siku tatu, mwisho wanafika kwenye mlima uliochaguliwa na Mungu. Abrahamu amewaambia watumishi hawa wawili wawaongojee, pamoja na mwana punda. Sasa ni Isaka ndiye amechukua kuni wakati baba yake anabeba Makala ya moto na kisu ***(Mwanzo 22:4-6)***<br>• Wakati weko wanapanda, Isaka anamuuliza baba yake mwana kondoo eko wapi kwa sadaka ya kuteketezwa. Abrahamu akamjibu: “Mungu atajipatia mwenyewe mwana kondoo.” ***(Mwanzo 22:7-8)***<br>• *Abrahamu alimtii Mungu sababu alimpenda. Mungu anataka kwamba tumpende kwa moyo wetu wote, na kwamba tumtii katika yote ambayo anatuomba kufanya.*<br><br>***Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.*** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***ao Mwanzo 22:8, ao Kumbukumbu la Torati 6:5***. Eleza maana yake ikiwa ni lazima. |
| **KURUDIA** | • Mwana wa Abrahamu aliitwa kwa jina gani?<br>• Mlima kule Mungu alitaka Abrahamu aende iliitwa kwa jina gani?<br>• Ni watumishi ngapi ambao walimsindikiza Abrahamu?<br>• Abrahamu alienda pamoja na nyama gani?<br>• Safari ya kuelekea mlima ilifanya siku ngapi?<br>• Kulingana na Abrahamu, ni nani ambaye alipaswa kujipatia mwenyewe mwana kondoo?<br>• Abrahamu alimpenda nani zaidi ya yote?<br>• Ni nani ambaye tunapaswa kumpenda kwa moyo wetu wote? |

## A6 SOMO 2
**Abrahamu anamtii Mungu**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Mungu alitoa kondoo ili afe pahali pa Isaka.<br>• Yesu alibeba fasi yetu ili afe msalabani kwa ajili ya zambi zetu<br><br>**Mstari muhimu:** ***Mwanzo 2:20***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 22:9-14*** |
| **KUTANGULIZA** | • Uwaambie watoto wajaribu kuwaza kwamba wataazibiwa sababu ya kosa fulani. Watajisikia namna gani ule wakati?<br>• Kisha wajaribu kuwaza kwamba mtu mwingine ataazibiwa pahali yao. Watajisikia namna gani?<br>• Eleza kwamba katika historia ya leo, kitu moja kinachukua fasi ya Isaka (katika mazabahu) |
| **KUFUNDISHA** | • Urudie pamoja na watoto katika historia tangu mwanzo mpaka sasa.<br>• Mwisho, Abrahamu na Isaka wanafika sasa pale juu ya mlima kwenye Abrahamu anajenga mazabahu kwa mawe. Ananamfunga Isaka na anamweka katika mazabahu ***(Mwanzo 22:9-10)***<br>• Wakati Abrahamu anajiweka tayari kwa kumtoa Isaka kwa Mungu kama sadaka ya kuteketezwa, malaika anamwuita toka mbingu na anamwambia asimame na asiweke mkono wake juu ya mwana wake. Abrahamu alionyesha mu kiwango gani alimpenda Mungu. ***(Mwanzo 22:11-12)***<br>• Abrahamu ananyanyua macho na anaona kondoo aliyekamatwa na pembe katika mti mfupi. Sasa anamtoa kodoo kama sadaka ya kuteketezwa pahali pa Isaka. ***(Mwanzo 22:13)***<br>• *Unawaza, Abrahamu na Isaka walifanya nini wakati walitambua kwamba kondoo atachukua pahali pa Isaka?*<br>• *Wakati Yesu alikufa msalabani, ilikuwa pahali yetu. Kwa kweli, sisi wote tulifanya vitu vibaya, lakini wakati Yesu alikufa alichukua mapigo ambayo tulistahili juu ya vitu hivi vibaya.*<br>• *Yesu alikufa kwa ajili yetu sababu alitupenda na hakutaki tuteswe kwa sababu ya mapigo ambayo tulistahili juu ya zambi zetu.*<br>• *Anataka kwamba sisi vilevile tumpende na kwamba tumshukuru aksanti kwa kubeba fasi yetu.*<br>• *Unajisikia je wakati unawaza kwamba Yesu alikupenda mu kiwango cha kutoa uzima wake kwa ajili yako?*<br>• *Namna gani tunaweza kuonyesha mapendo yetu kwa Yesu?*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Wagalatia 2:20***. Eleza maana yake ikiwa ni lazima. |
| **KURUDIA** | • Mazabahu ambayo Abrahamu alijenga ilikuwa wapi?<br>• Aliijenga na nini?<br>• Ni nani alimwita toka mbingu?<br>• Malaika alimwambia nini Abrahamu?<br>• Abrahamu alionyesha nini kwa Mungu?<br>• Ni nyama gani ambaye alichukua fasi ya Isaka katika mazabahu?<br>• Ni nani ambaye alichukuia fasi yetu msalabani?<br>• Kwa nini Yesu alikufa msalabani? |

**A6 SOMO 3**
**Msaada wa Mungu**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Mtumishi aliomba msaada kwa Mungu na Mungu alimsaidia.<br>• Mungu atatusaidia, didi pia, ikiwa tunamuomba.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Mwanzo 24:27, Matayo 7:7***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 24:1-28*** |
| **KUTANGULIZA** | • Uwaambie watoto wafikirie kuhusu watu ambao wanawasaidia. Ni nani anakusaidia? Watu hawa wanakusaidia kwa nini? Unajisikia je wakati wanakusaidia?<br>• Uwape watoto wakati waseme jinsi gani waliweza kusaidia mtu?<br>• Uwaambie kwamba, katika somo ya leo, Mungu anasaidia mtu. |
| **KUFUNDISHA** | • Sasa Abrahamu ni mzee sana, lakini mbele ya kufa, anataka kuhakikisha kwamba Isaka anaoa na ni mwenye heri. Anampa sasa mtumishi wake mkubwa maagizo, ili huyo amtafutie mtoto wake bibi. Anamwambia amtumainie Mungu kwa kumuongoza kwenye mtu mwema. ***(Mwanzo 24:1-9)*** *Mtumishi huyu aliwaza nini wakati Abrahamu alimwambia amtafutie Isaka bibi?*<br>• Mtumishi anachukua ngamia kumi za bwana wake na anaenda. Kisha kusafiri muda wa siku nyingi, anasimama karibu na kisima kimoja katika mji wa Nahori. Sasa ni mangaribi, na wa binti wote wanatoka ili watafute maji kwenye kisima. ***(Mwanzo 24:10-11)***<br>• Ni pale sasa mtumishi anamwomba Mungu ili amuonyeshe kama mmoja wa wabinti hawa atakuwa bibi wa Isaka. Atawaomba maji ya kunywa, na ikiwa mmoja wao anampatia maji ya kunywa na anatoa pia maji kwa ajili ya ngamia zake kumi, sasa atatjua kwamba ni yeye atakuwa mke wa Isaka. ***(Mwanzo 24:12-14)***<br>• Baada ya muda kidogo, anaona binti mmoja mzuri sana anakaribia kwenye kisima. Jina lake Rebeka. Wakati anamwomba maji ya kunywa, anampa maji kwa haraka, na anashota pia ya wa ngamia. *Mtumishi anapaswa kuwaza nini ule wakati? Anapaswa kujisikia je?* ***(Mwanzo 24:15-21)***<br>• Kisha kumpa zawadi kutoka kwa bwana wake Abrahamu, anamuuliza kama kwa baba yake kuna fasi ya kutosha juu ya kulala. Anaitika. Sasa mtumishi anainama na kuabudu Mungu ambaye anajibu maombi yake na anamsaidia kupata binti *mwema.* ***(Mwanzo 24:22-27)***<br>• *Umekwisha kupata kazi ambayo ni ngumu kuitimiza? Toa mifano ambayo inaweza kueleweka kwa kundi lako.*<br>• *Mtumishi huyu aliomba msaada kwa nani?*<br>• *Na sisi, tunaweza kuomba msaada kwa nani? Mungu anataka kutusaidia na kutuongoza wakati tunachagua na tuko na maamuzi ya kufanya. Atatuongoza kuchagua mzuri na kuamua mzuri.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***ao Mwanzo 24:27, ao Matayo 7:7***. Eleza maana yake ikiwa ni lazima. |
| **KURUDIA** | • Ni nani ambaye alienda kumtafutia Isaka bibi?<br>• Ni wa ngamia ngapi ambao walimsindikiza mtumishi huyu?<br>• Mtumishi huyu alisimama wapi?<br>• Ilikuwa saa ngapi ya mchana?<br>• Mtumishi alimwomba nani msaada ili apate bibi aliyekusudiwa juu ya Isaka?<br>• Binti ambaye alikuwa kwenye kisima, jina lake ilikuwa nani?<br>• Alifanya nini kwa kumsaidia mtumishi?<br>• Mtumishi alifanya nini wakati alitambua kwamba Mungu alimsaidia?<br><br>Ikiwa kunabaki muda wa kutosha, watoto wanaweza kuchora picha pale wanasaidia mtu. |

**A6 SOMO 4**
**Kuchagua kwa Mungu**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kwamba:**<br>• Rebeka na Isaka walifuata mpango wa Mungu na ile iliwafanya kuwa na heri.<br>• Ikiwa tunamtumainia Mungu na tunafuata ma njia zake, tutakuwa wenye heri.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Zaburi 144:15***<br>**Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 24:28-67*** |
| **KUTANGULIZA** | • Uwaulize watoto kama wamekwisha kuhuzuria katika ibada ya ndoa. Ni wa nani walioana? Walivaa mavazi ya namna gani? Ndoa ilifanyika namna gani? Walioolewa walijisikia kuwa na heri?<br>• Uwaambie watoto kwamba somo ya leo ni kuhusu ndoa moja ya nyakati za Biblia. Pengine haifanane na ndoa ya leo katika inchi yenu. |
| **KUFUNDISHA** | • Uwakumbushe watoto ile inafanyika mpaka sasa katika historia hiyo.<br>• Rebeka alienda mbio nyumbani kuwaambia familia yake ile iliyofanyika. Kaka yake Labani alienda mbio kwenye kisima, na alimleta mtumishi huyu nyumbani, akamkaribisha vizuri. Lakini kabla ya mtumishi kula chakula, aliambia familia ya Rebeka sababu ya safari yake. ***(Mwanzo 24:28-49)***<br>• Baba wa Rebeka, pia Labani, wamehakikishwa wote wawili kwamba ni Mungu ambaye alimwongoza mtumishi wa Isaka kwa Rebeka. Bila kusita walimpa ruhusa ya kumpeleka Rebeka ili awe bibi wa Isaka. Mtumishi alimshukuru Mungu juu ya jibu ya ombi yake. Kisha, alitoa zawadi nyingi kwa Rebeka na famila yake. ***(Mwanzo 24:50-53)***.<br>• Asubui iliyofuata, wanamuuliza Rebeka kama yeye ni tayari kwenda na mtumishi ili aolewe na Isaka. Rebeka anakubali. ***(Mwanzo 24:54-61)*** *Rebeka anajisikia je wakati huu? (Bila shaka ni woga kidogo sababu hajui Isaka na familia yake, lakini alikuwa pia haraka sababau alielewa kwamba ni Mungu ambaye alipanga mambo yote!)*<br>• Wakati huu, Isaka anaongojea katika nyumba ya baba yake Abrahamu, akijiuliza ni nini inaweza kufanyika kweli. Siku moja mangaribi, wakati alikuwa anafikiria kwenye shamba ya shamba, anaone ngamia zinakuja. Baada ya muda kidogo, anampokea Rebeka ndani ya nyumba yake mpya, na anamwongoza kwenye hema ya mama yake. Isaka anampenda sana Rebeka na huyo anakuwa bibi yake. ***(Mwanzo 24:61-67)***<br>• *Isaka anajisikia je wakati anaona bibi yake mara ya kwanza? (Bila shaka anafurahi, na pia eko na wasiwasi sababu alikuwa bado kukutana naye kabla, lakini tena yeye anatumainia mpango wa Mungu. Mungu anataka kwamba, sisi pia, tumtumainie, na tufuate mipango yake. Kwa hiyo tutapata furaha na heri.*<br><br>**Kusoma na kujaza somo wakati wa Biblia.** |
| **KUJIFUNZA** | Kujifunza mstari muhimu, ***Zaburi 144:15***. Mstari huu unaonyesha furaha tunayopata wakati Mungu anatimiza mipango yake katika maisha yetu. |
| **KURUDIA** | • Kaka yake ya Rebeka alikuwa anaitwa nani?<br>• Mtumishi huyu alifanya nini kabla ya kula chakula?<br>• Kwa nini familia ya Rebeka iliruhusu kwamba awe mke wa Isaka?<br>• Mtumishi huyo alitoa nini kwa Rebeka na familia yake?<br>• Kulingana na wao, ni nani ambaye alimwongoza mtumishi huyo kwa Rebeka?<br>• Rebeka na mtumishi huyo walienda wakati gani?<br>• Ni nani alitoka katika shamba wakati Rebeka na mtumishi huyo walikuja?<br>• Kwa nini Isaka na Rebeka walifurahi wakati walikutana?<br>• Ni nani ambaye anaweza kutupa furaha zaidi kuliko mtu yeyote ao kitu chochote? |

## Mashauri kwa wakufunzi wa masomo

**KIWANGO 1:**

- Ukurasa moja (mbili katika vitabu) kwa wiki ambayo zaidi kuna kazi ya kupaka rangi na maneno kidogo ya kuandika.
- Pointi kumi zimewekwa kwa wiki, na kiwango cha juu cha pointi 40 kwa mwezi.
- Pointi mbili imewekwa kwa kila jibu inayofaa yenye kuandikwa na ma pointi inayobaki imewekwa juu ya kupakaa rangi. Yote pamoja inafanya kiwango cha ma pointi 10 kwa kila somo katika wiki.
- Ni kawaida kwamba watoto wanaojifunza masomo za kiwango 1 hawajue bado kusoma vema. Watahitaji msaada wa wazazi wao ao walimu.

**KIWANGO 2:**

- Ukurasa mbili (ine katika kitabu) kwa wiki.
- Historia ya Biblia inaelezwa katika somo. Watoto wanapaswa kupata maneno ya somo, kupaka rangi, kujaza mstari muhimu, na vivyo hivyo.
- Ma pointi 20 imewekwa kwa wiki, na kiwango cha juu cha ma pointi 80 kwa mwezi.

**NAMNA GANI KUREKEBISHA MASOMO?**

- Kuangalia kila ukurasa kwa kuchunguza majibu.
- Kuleta ma pointi kulingana na majibu.
- Kutumia kalamu ya rangi tofauti na ile mtoto alitumia.
- Ongeza, ikiwa ni lazima, jibu inayofaa na kurekebisha makosa ya herufi (lakini hiyo haiwezi kupunguza kiwango cha pointi).
- Kupatia ma pointi kidogo kwa jibu isiyo ya kutosha kabisa ao ya kipande.
- Kuhesabu jumla ya ma pointi kwa mwezi na kuiandika katika ukurasa wa mwisho, pa fasi iliyotayarishwa.

Ni ya muhimu kuwa mwema katika namna ya kupana ma pointi na kufanya yote iwezekanayo kwa kuwatia moyo watoto katika majifunzo yao ya Biblia. Usisite kusema neno ya kutia moyo, sifa, katika sanduku iliyopangwa kwa ajili ya ile ukiandika kwa mfano rangi ilipakwa mzuri, usafi wa kazi, ma pointi iliyopewa, uelewa mzuri wa mafundisho, vivyo hivyo. Ni ya muhimu kwa mtoto kuwa mwangalifu kweli ili a tofautishe maoni. Maswali, maoni, misemo ya kutia moyo inaamsha akili ya mtoto. Lakini, kama ni misemo hiyo hiyo inarudiwa mara kwa mara, kwa wepesi itapoteza bei yake.

**KIWANGO 1**

**Maoni kwa jumla:**

“Isabelle ninafurahi hivi unaanza masomo hii na ninatumaini kwamba itakupendeza. Kupakaa rangi kwako ni nzuri sana ! je unaenda shule ? Uniambie ! Nitafurahi kupata habari yako.”
“Kazi nzuri Anderea. Rangi mzuri! Ilikuwa mgumu kwa kufanya? Ulisahau kidogo katika somo ya mwisho.”

**Maoni ya kiroho:**

“Vizuri, Sara ! Yairo alipaswa kufurahi sana wakati Yesu alimsaidia.”
“Jibu mzuri sana! Historia ya kifo cha Yesu ni ya huzuni sana, lakini alifufuka. Hii ni habari njema!”

**KIWANGO 2**

**Maoni kwa jumla:**

“Kazi mzuri, kama vile kila mara, Joanna. Nina uhakika wa kwamba mwalimu wako shuleni anafurahi pia juu ya kazi yako!
“Ninaona kwamba ni sasa hivi kumbukumbu ya kuzaliwa kwako, Simoni. Ulitayarisha kitu gani cha kipekee? Kweli, siku iwe njema kwako!”
“Ulijikaza kabisa. Kuna makosa kidogo. Usisahau kusoma majibu yako kila mara.”

**Maoni ya kiroho:**

“Ninapenda sana jinsi ulimpakaa rangi mtoto Yesu rangi katika sanduku ya chakula. Mungu alionyesha mapendo yake kweli kwa kumtuma katika dunia, sivyo?
”Rangi zako ni nzuri! mambo ilikuwa mbaya kwa Zakaria sababu ya kutokuamini mambo ambayo Mungu alimwambia! Baadaye hakuwe tena na shaka ya neno la Mungu.”
“Ma jibu mzuri sana! Mtu aliyekuta filipo katika jangwa alirudi na furaha. Alisikia na kuamini habari njema ya Yesu.”

© Bible Educational Services 2019

www.besweb.com

Registered Charity UK CIO 1186004

Congo-Swahili   SWC

07/2024